# Nipashe

Jumamosi Februari 6, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580483

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710





**SHERIA** ya Ndoa sasa kufumuliwa

UKURASA 5



**SABABU** wanaume wenye VVU kufa mapema yatajwa

UKURASA 9

UKURASA 11

# Usajili nyumba zote unakuja



UKURASA 2



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta (kulia), akiongoza waombolezaji kuaga mwili wa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa huo, Richard Kwitega, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini humo jana, na baadaye kusafirishwa kwenda Kijiji cha Ngoma, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, kwa mazishi yanayotarajiwa kufanyika leo. Kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Jengo lililoporomoka laponza vigogo Z'bar

UKURASA 10

UKURASA WA 3

## TAKUKURU KUCHUNGUZA MALIPO KIPIMO CHA MKOJO

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Kwala Halmashauri ya Kibaha Vijijini, wameiomba Taasisi ya Kuzuia na ...

UKURASA WA 7

## RC AONYA WAZAZI UBAKAJI WA WATOTO

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewaonya wazazi na walezi mkoani humo kuhusu tabia ya kulaza wageni kwenye vyumba vya...

## GWAJIMA ALIAMSHA 'DUDE' BUNGENI

UKURASA 2

**MICHEZO** **GOMES AIPIGIA HESABU YANGA** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Usajili wa nyumba waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekuja na mbinu mpya za kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya majengo yanayopaswa kulipiwa kodi kwa mujibu wa sheria, kwa kuzitambua na kukusanya takwimu za majengo yote nchini zitakazoonyesha jina la mmiliki au msimamizi na namba yake ya simu, ili kurahisisha makusanyo.

Utambuzi wa majengo hayo ulianza jana na utatekelezwa hadi Februari 28, mwaka huu na ripoti yake kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ifikapo Machi 4 mwaka huu na utaenda sambamba na kampeni maalum ya ukusanyaji kodi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Hatua hiyo inatokana na tamko la serikali lililotolewa siku chache zilizopita kuhamisha ukusanyaji wa kodi hiyo pamoja na ushuru wa mabango kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) na kurudishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyokuwa awali.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Selemani Jafo, alitoa maagizo hayo jana katika kikao kazi cha kutoa maelekezo mahsusi ya serikali kuhusu ukusanyaji kodi hiyo, ushuru wa mabango na usimamizi wa ugawaji wa vitambulisho vya mjasiriamali, kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri nchini.

Jafo alisema kodi ya majengo haijakusanywa vizuri, hivyo kwa mikakati iliyopo ya serikali, inataka ikusanywe ipasavyo ambapo hadi Machi 4 mwaka huu, serikali itakuwa na takwimu za majengo yote nchini.

"Ninataka nione tunakusanya kodi hii kihistoria kuanzia sasa hadi Februari 28 mwaka huu, ndani ya wiki hizi tatu zitumike kukusanya taarifa na kutambua majengo yote yaliyopo kwa kila mtaa, tunataka taarifa za majengo yanayopaswa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria isipokuwa zile za matope," alisema.

Aliagiza kila Ofisa Mtendaji wa Mtaa au Kijiji ahakikishe anakusanya takwimu za majengo yaliyoko kwenye eneo lake na zihakikiwe na Ofisa Mtendaji wa Kata na baadaye kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika ili kuwasilishwa TAMISEMI ifikapo Machi 4, mwaka huu.

"Mkurugenzi kazi yako ya kwanza ni kila mtendaji wako wa mtaa akupatie takwimu, kuna nyumba za aina gani kwenye mtaa wake ambazo zimesainiwa pia na mwenyekiti wa mtaa, taarifa ziainishe aina na jina la mmiliki au msimamizi wa nyumba na namba yake ya simu, tutakuwa na kanzidata ya kihisitoria," aliagiza.

Alisema kutakuwa na kampeni maalum ya ukusanyaji kodi hiyo ambayo itaanza Machi 22 hadi Aprili 5 mwaka huu, huku akiwataka wale wote ambao hawajalipa kodi ya mwaka 2020/21 kuhakikisha wanalipa na risiti za kielektroniki (EFDs) zitolewe kwa walipaji.

"Ni kampeni maalum ya ukusanyaji wa kodi ya majengo, zoezi litaendeshwa nchi nzima, wale waliolipa wataonyesha risiti zao na wale ambao hawajalipa, tunatarajia tutakapofunga, watakuwa wamelipa na hii ndio staili yetu ya kwanza," alisema.

Jafo alisema ushuru wa mabango umeonekana haukusanywi vizuri na serikali imetoa maelekezo ya namna ya kukusanya.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, alisema lengo la kikao hicho ni kutoa maelekezo mahsusi ya ukusanyaji wa kodi ya majengo, ushuru wa mabango na usimamizi wa ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali.

"Mwaka jana ugawaji wa vitambulisho ulikuwa asilimia 40, tulichelewa kugawa lakini na Uchaguzi Mkuu, mwaka huu tunataka tufanye vizuri na vitambulisho kwa mwaka huu vimechapishwa milioni 1.6 na TRA kwa taarifa waliyonipa vimeshafika kwenye ofisi za mikoa, mtapewa orodha kujua kila mkoa umepata vitambulisho kiasi gani," alisema.

Alisema vitambulisho hivyo vimeboreshwa ambapo mjasiriamali ataweka picha na hatua hiyo imeepusha tabia ya kitambulisho kimoja kutumika na wafanyabiashara zaidi ya mmoja.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Adolf Ndunguru, alisema katika ukusanyaji wa kodi hiyo, zipo kero zilizojitokeza na serikali kulazimika kutoa maelekezo ya ukusanyaji wa kodi hiyo licha ya kuwa chini ya usimamizi wa TRA.

"Ufanyike ushirikishwaji wa kutosha wa TAMISEMI ili kukusanya kodi hiyo ipasavyo," alisema.

## Gwajima aliamsha 'dude' bungeni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wabunge kuibana serikali iongeze bajeti ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kutoka mgao wa sasa wa asilimia 30 hadi kufikia asilimia 40, akionya kuwa wasipofanya hivyo, hawatarudi bungeni baada ya miaka mitano.

Kabla ya Ndugai kuipigia chapuo TARURA kuongezwa fedha, Mbunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, maarufu 'mzee wa kuliamsha dude', alisema hakuna mateso waliyonayo wabunge kama TARURA kukosa fedha.

Askofu Gwajima alikuwa anachangia mjadala wa hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la 12 Novemba mwaka jana.

Akikazia hoja ya mbunge huyo, Spika Ndugai alisema: "Sasa, safari hii hebu hili tulishike sasa kama wabunge, maana vinginevyo hamrudi.

"Nyie chekeni tu na TARURA. Barabara zote mpaka hapa Jiji la Dodoma ni TARURA, Mwanza TARURA ipo, yaani yenyewe iko vijijini na mijini. Kwani Kawe ni wapi? Kwa hoja hiyo, kwa kweli haiwezekani, hela haitoshi lakini 'kamgao kawapo kawapo' hivi.

"Hatusemi iwe nini, lakini basi iongezewe bajeti hata iwe asilimia 40, lakini lazima kufanyike kitu, hatuwezi kuendelea hivi, haiwezekani."

Spika Ndugai, alisema ni lazima ifike mahali waliamue jambo hilo kwa ajili ya manufaa ya muda mrefu.

"Itakuwa muda wa wabunge ni kuongelea jambo hilo hilo moja kila siku, kidogo inakuwa haifai. Kwa hiyo, ni jambo la kulitazama katika bajeti ya mwaka huu. Tuangalie hiyo fomula kama ina shida kwenye sheria au ilikuwa wapi inahitaji iangaliwe kwa kweli.

"Ni kilio cha miaka mingi na wabunge wengi hawarudi, lakini kero zao kubwa ni barabara, wabunge wanaanguka, wanakuja wapya kisa TARURA," alisema.

Katika mchango wake, Askofu Gwajima alisema TARURA haileti maana ukiona mtandao wa barabara za wakala huo kilomita 130,000 kulinganisha na mtandao wa barabara za TANROAD kilomita 40,000.

Alisema haileti maana kwanini mpaka sasa wakala huo unapewa asilimia 30 na TANROAD anapewa asilimia 70 ya fungu la barabara.

"Hakuna mateso tuliyonayo wabunge kama TARURA kukosa fedha kule mikoani, ni ngumu sana. Nitoe mfano kwenye jimbo langu la Kawe.

"Wilaya nzima ya Kinondoni tuna kilomita za barabara za ndani 1,663. Kilomita 200 ziko Jimbo la Kinondoni kwa pacha wangu Abassi Tarimba, kilomita 1,463 ziko Jimbo la Kawe na ni sawasawa kukosa Dar es Salaam mpaka Kigoma, lakini zote ziko ndani ya Jimbo la Kawe," alisema.

Askofu Gwajima alisema alipowatembelea TARURA, walimweleza wanazo fedha za kutengeneza kilomita 120,000 pekee, ikiwa ina maana kuna kilomita 1,300 ambazo haziwezi kutengenezwa.

"This is not acceptable (haikubaliki) katika nchi yetu na kama kweli tuna ndoto ya kuwaletea watu maendeleo kwa nchi yetu na sio Jimbo la Kawe tu. Barabara zinazotakiwa kujengwa kwa kutumia fedha za TARURA hazitajengwa kabisa kama TARURA hataongezewa fedha.

"Ninaomba watendaji wawaze mawazo mengine tena ya kuongezea fedha, wasitegemee mawazo yale yale ya John Magufuli, alipokuwa Waziri wa Ujenzi," alisema.

### WAKALA UFUTWE

Mbunge wa Sindida Kaskazini (CCM), Ramadhan Ighondo, akichangia mjadala huo, alisema wamechoka na wanachozungumza wabunge ni maisha halisi yaliyopo kule kwenye maeneo yao.

"Ninashauri kama hii TARURA haitapewa fedha, basi ifutwe. Kwa sababu hizo ni kodi za Watanzania, majengo wanayojenga kila wilaya nchi hii, hata lile jengo lao pale wizarani, hizo ni kodi za Watanzania.

"Hizo fedha badala ya kutumiwa kwenye mafuta, kwenye majengo na kwenye viti na kwenye mishahara, zichukuliwe zipelekwe zikatengeneze barabara," alisema Ighondo.

### 'FORCE ACCOUNT'

Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Maasai, alisema katika jimbo lake kuna kilomita 1,300 za TARURA, lakini wanapata Sh. milioni 6,66 ambazo haziwezi kutengeneza barabara.

"Wakati tunatunga sheria ya kuisaidia serikali kutumia mfumo wa kumudu soko kwa kuja na utaratibu 'force account' (mafundi jamii), niombe serikali ije na mpango wa kuisaidia TARURA.

"Inawezekana tunapigwa sana na makandarasi. Sasa ili kuisaidia, twende kwenye force account pia kwenye TARURA," alisema Maasai.

Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota, aliomba serikali kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kuuongezea fedha wakala huo ufanye kazi yake kwa ufanisi.

"Barabara yetu ya ulinzi, niipongeze kamati yetu ya ulinzi na usalama kwa kufanya kazi nzuri kwenye mpaka wa Tunduma, sasa ninaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara hadi Mbinga, ni barabara muhimu kwa ulinzi na usalama wa nchi," alisema.

Mbunge wa Singida Mashariki, Miraji Mtaturu (CCM), alishauri TARURA kutengewa fedha za kutosha ili wakala huo ufanye kazi kwa ufanisi.

"Katika miundombinu ya barabara, TANROAD inafanya vizuri kwa sababu imewezeshwa, tulivyoamua kuanzisha TARURA, lengo lilikuwa ni kuondoa urasimu uliokuwapo wa kuleta fedha kupitia mfuko wa barabara.

"Leo hii tunavyoleta mgawanyo wa asilimia 70 kwa TANROAD na asilimia 30 kwa TARURA, tunaifanya taasisi hii ishindwe kufanya kazi yake na inakuwa haina maana kuianzisha, niombe TARURA iongezewe fungu," alisema.

Jana asubuhi, wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Naibu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema mwaka 2019/20, bajeti ya TARURA ilikuwa Sh. bilioni 241 na mwaka 2020/21 imeongezeka na kufikia Sh. bilioni 275, sawa na ongezeko la Sh. bilioni 34.

"Ni kweli TARURA ina mzigo mkubwa wa barabara ambazo ni kilomita 108,496 za barabara, lakini bado bajeti haitoshelezi ingawa serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na zimekuwa zikiongezeka kulingana na bajeti.

"Serikali inaona sababu ya kutafuta vyanzo vingine vya kuongezea uwezo TARURA ili ifanye majukumu yake vizuri," alisema.

Naibu Waziri huyo alikuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, aliyetaka kujua serikali haioni haja ya kuanzisha chanzo maalumu kwa ajili ya TARURA badala ya kutegemea Mfuko wa Barabara.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU kuchunguza malipo kipimo cha mkojo

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Kwala Halmashauri ya Kibaha Vijijini, wameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia tatizo la Zahanati ya Kwala kukosa kipimo cha mkojo na badala yake kuwekwa cha mtu binafsi.

Fatuma Mgaza, ambaye ni mkazi wa Kwala alieleza kero hiyo kwenye mkutano ulioandaliwa na TAKUKURU kusikiliza kero za wananchi ambapo kati ya malalamiko yaliyoelezwa ni pamoja na kero ya kulipia kipimo hicho kinachodaiwa ni cha mtu binafsi.

Mwananchi huyo alisema wanapokwenda katika zahanati hiyo na kutakiwa kupima mkojo wanaambiwa kwamba hakuna vikinga mkono (gloves) na hivyo kutakiwa kulipa Sh. 4,000 pamoja na gharama za kipimo cha mkojo.

"Tukifika wanasema hakuna vikinga mkono tulipie Sh. 1,000 na kwa kipimo cha mkojo ni Sh. 3,000, tunaambiwa kipimo hicho siyo cha zahanati ni mali ya mtu binafsi kinatakiwa kulipiwa ndipo tupate huduma ya kupimwa," alilalamika Fatuma.

Akizungumzia suala la dawa, mwananchi huyo alisema pamoja na kukata bima, lakini hawapati dawa kwani baada ya kuandikiwa wanatakiwa kwenda kununua wenyewe jambo ambalo linawafanya ambao hawana bima kukosa mwamko wa kukata.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Zaka Msafiri, alisema atafuatilia jambo hilo ili pate ukweli wake.

Naye Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Suzana Raymond, alielezea kushangazwa na utaratibu huo na aliahidi kuwa yeye na watendaji wa ofisi yake watashughulikia suala hilo kwa haraka.

# Serikali yaahidi kuipaisha sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema katika kipindi cha muhula wa pili wa miaka mitano ya Rais John Magufuli, Tanzania itajikita zaidi katika diplomasia ya uchumi, kuimarisha sekta binafsi, kukuza biashara pamoja na uhusiano na mataifa mbalimbali duniani.

Msimamo huo wa Tanzania ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, wakati wa mkutano wake na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini na wakuu wa mashirika ya kimataifa.

Prof. Kabudi alisema ni dhamira ya Tanzania kuhakikisha kuwa ina uwezo wa kukuza biashara na kuuza bidhaa katika nchi mbalimbali duniani.

Kabudi aliwaambia mabalozi na wakuu wa mashirika ya kimataifa hapa nchini kuwa hali ya kisiasa na amani Zanzibar na Tanzania kwa ujumla imeimarika kuliko wakati wowote husussani baada ya Uchaguzi Mkuu uliomalizika Oktoba 2020.

Alisema kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar kunachochea kuongezeka kwa uwekezaji na ufanyaji wa biashara kwa lengo la kukuza uchumi.

Kwa upande wake, kiongozi wa mabalozi hao, Dk. Ahmada El Badasui `Fakih ambaye pia ni Balozi wa Comoro hapa nchini, alishukuru uwepo wa mkutano huo, ambao unawapa fursa mabalozi kufahamu masuala mbalimbali yanavyoendelea hapa nchini. Balozi wa Umoja wa Ulaya, Manfredo Fanti, aliipongeza Tanzania kwa kuingia uchumi wa kati na kwamba Umoja wa Ulaya uko tayari kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha uchumi wa Tanzania unaendelea kukua.

Mkutano huo wa mabalozi na wakuu wa mashirika ya kimataifa umehudhuriwa pia na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, William Tate Ole Nasha, Katibu Mkuu Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na vitengo vya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.




Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Kisarawe Ushoroba, jana, litakalotangaza vivutio vya utalii vilivyopo kwenye Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia wa Kazimzumbwi, tamaduni za Wazaramo na Hifadhi mpya ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, litakaloanza Februari 19, mwaka huu, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani. Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (katikati) na Mhifadhi Mwandamizi Idara ya Utalii wa Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, Seth Mihayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vifaa vya umeme vyaanza kutengenezwa nchini

**Na Romana Mallya**

UWEKEZAJI mkubwa unaofanywa na Kampuni ya Elsewedy Elektroniki ya kuzalisha transfoma, mita za umeme na nyaya unaoendelea Kigamboni utaiwezesha Shirika la Umeme (Tanesco) kuongeza kasi ya uunganishaji umeme kwa wananchi na viwandani.

Mradi huo ambao unagharimu Dola za Marekani milioni 50 ni ule ambao Rais John Magufuli alitoa maelekezo ya kuhakikisha unafanikishwa haraka iwezekanavyo baada ya kuwapo kwa taarifa za ucheleweshaji ikiwamo upatikanaji wa ardhi.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk. Tito Mwinuka, walitembelea eneo la mradi na kujionea kazi ya ujenzi ikiendelea eneo hilo huku uzalishaji ukitarajiwa kuanza mwezi Juni, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, Dk. Kazi alisema uwekezaji huo unafanywa na wawekezaji kutoka nchini Misri ambao wamekuwa Tanzania kwa miaka miwili.

"Kuna vitu vilikuwa vina simama kidogo, lakini tumefanikiwa kuongea na taasisi zinazohusika ili ziongeza kasi ya kuwapatia mahitaji yao, wameshapata ardhi hii yenye ukubwa wa kilomita za mraba 120,000 ambazo wanawekeza mradi wao wa vifaa vya umeme," alisema.

"Watazalisha nyaya, transfoma na vifaa vingine vya umeme ambavyo vitaifanya Tanzania ijitosheleze na kupata ziada ya kuuza nje ya nchi na kupata fedha za kigeni na Watanzania wengi watapata ajira," alisema.

Dk. Kazi alisema yapo maendeleo makubwa ambayo yataletwa na wawekezaji hao ambao wataifanya Tanzania kuwa makao makuu ya uzalishaji wa vifaa hivyo vya umeme.

"Wazo la kuifanya Tanzania kuwa makao makuu yao lilikuja baada ya kujadiliana nao kwa sababu walitaka kupeleka mradi huu nchi jirani, lakini baada ya majadiliano na kuwaeleza vivutio vilivyopo na utayari wetu wa uwekezaji mkubwa baadaye," alisema.

Dk. Kazi alisema wawekezaji hao wataleta teknolojia mpya kupitia uwekezaji huo ambapo watatumia roboti kutengeneza matangi ya transfoma ambayo yanahitaji umakini wa hali ya juu.

"Wanatakiwa kuboresha transfoma wanazolisha ili ziweze kushindana katika soko la kimataifa, teknolojia hii haina maana kwamba Watanzania hawatapata ajira, wataanzisha Chuo cha VETA ambacho kitakuwa kinawafundisha watu kuziendesha hizo roboti na kwa kuanzia wataajiri watu 250 mpaka 400," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk. Mwinuka, alisema kiwanda hicho kitakapoanza kazi kitazalisha mita za umeme, transfoma pamoja na nyaya vifaa ambavyo shirika linavihitaji.

"Tanesco ni wadau na wanufaika na kama shirika tunaendelea kutekeleza maelekezo ya serikali yanayotutaka tutumie vifaa vyote vinavyozalishwa nchini kwa ajili ya miradi tunayoitekeleza ya kusambaza umeme," alisema.

Dk. Mwinuka alikihakikisha kiwanda hicho kuwa soko la vifaa vya umeme Tanzania lipo na kwamba miradi mingi inakuja ikiwa ni pamoja na kuwaunga wateja wapya kila mwaka. "Kwa uzoefu wetu tangu tumeanza kununua vifaa hivi hapa nchini, kasi ya kuunga wateja imeongezeka kwa sababu ya urahisi wa upatikanaji wa vifaa, tunawashukuru Elsewedy kwa kuunga mkono shughuli zetu."

"Kwa mwaka huu katika miezi sita ya kwanza, tayari tumezidi idadi ya wateja tuliokuwa tukiwahudumia kwa mwaka mzima siku za nyuma," alisema.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo ya Elsewedy Afrika Mashariki, Ibrahim Qamar, alisema uwekezaji huo unagharimu Dola za Marekani milioni 50 na utakapokamilika utatoa ajira 395.

# Lukuvi aagiza Kiswahili kitumike mabaraza ardhi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewaagiza wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya, kutumia Kiswahili katika kuandika hukumu.

Lukuvi alitoa maagizo hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na wenyeviti na wasajili wa mabaraza hayo nchi nzima kupitia mkutano uliofanyika kwa mtandao.

"Ninasisitiza wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya, mtumie lugha ya Kiswahili wakati wa kuandika hukumu zenu kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais Dk. John Pombe Magufuli na nitashangaa kumwona mwenyekiti asiandike hukumu kwa lugha ya Kiswahili," alisema Lukuvi.

Aliwataka wenyeviti hao wa mabaraza kuchapa hukumu za uamuzi wanaotoa wao wenyewe bila kutegemea makarani na hukumu hizo zitoke kwa wakati na kusisitiza kuwa katika dunia ya leo suala la uzembe halina nafasi.

Waziri huyo aliongeza kuwa, pamoja na kuwapo uchache wa watumishi kwenye baadhi ya ofisi za mabaraza hayo, watendaji hao wanatakiwa kuwajibika na kuacha visingizio na kufanya kazi kwa mazoea kwa kuwa serikali iko katika juhudi za kuhakikisha inajaza nafasi hizo.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hivi sasa ni wajibu wa watendaji wa mabaraza ya ardhi kufanya kilicho sahihi na kuwa wabunifu na kuwajibika kwa kutoa hukumu kwa wakati na kusisitiza wananchi maskini wanategemea matumizi ya Kiswahili.

"Uamuzi wetu kama wenyeviti wa mabaraza uwe rahisi na sisi tuwe wa kwanza na kila mwenyekiti atekeleze uamuzi huu kwa lugha ya Kiswahili," aliagiza.

Lukuvi alibainisha kuwa wapo wananchi waliokosa haki zao ama kuchelewa kukata rufani kutokana na kutokujua kilichoandikwa katika hukumu kwa kuwa kimeandikwa kwa Kiingereza.

Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Stella Tullo, aliwataka wenyeviti wa mabaraza hayo kuanza kutekeleza maagizo ya waziri mapema kwa kuzingatia sheria na taratibu.



Washtakiwa wa makosa matatu yakiwamo ya kupatikana na vipande 32 vya bidhaa zilizotengenezwa na meno ya tembo na tisa ya Simba, vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 45, wakiwa chini ya ulinzi wa polisi, baada ya kusomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madiwani wacharuka miradi kutekelezwa chini ya kiwango

**Anthony Gervas,** MAGU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, wameulalamikia Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani humo kwa kutekeleza miradi ya barabara chini ya kiwango kinachotakiwa.

Walitoa malalamiko hayo juzi katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, kilichofanyika mjini Magu.

Madiwani hao waliiomba serikali kuuondoa wakala huo katika shughuli za utengenezaji wa barabara hizo.

"Tunaiomba serikali kuuondoa wakala huu ambao unafanya kazi za ujenzi wa barabara chini ya kiwango na kusababisha kutuchonganisha na wananchi sisi madiwani," alisema Lucas Mchibula, mmoja wa madiwani hao.

Hoja hiyo iliungwa mkono na madiwani wote katika baraza hilo, huku wakidai kuwa barabara nyingi zinajengwa chini ya kiwango.

Waliitaka serikali kuirudisha miradi hiyo chini ya usimamizi wa halmashauri ya wilaya hiyo, ili madiwani na watendaji wengine wa serikali waisimamie na kuondoa lawama kwa wananchi.

Akifafanua hali ya kutofanya vizuri katika ujenzi wa barabara hizo, Meneja wa TARURA wilayani humo, Leonidas Sospeter, alisema kasoro hiyo imetokana na kuwapo kwa upungufu wa watumishi.

Leonidas alisema wamefanikiwa kulipa madeni yote ya ujenzi wa barabara waliyokuwa wakidaiwa na kuahidi kutekeleza shughuli za ujenzi huo kwa ufanisi.

## Katibu Mkuu: Serikali itaendeleza wabunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kuendeleza wabunifu 130 kati ya 1,066 wa nyanja mbalimbali walioibuliwa katika mashindano ya kitaifa ya sayansi teknolojia na ubunifu (MAKSATU), ili ubunifu wao uendelee kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Katibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema wabunifu hao walipatikana katika mashindano hayo yaliyofanyika miaka ya nyuma.

Dk. Akwilapo alisema serikali inafanya hivyo ili kuhakikisha inaendeleza kazi za wabunifu ambazo zimeonekana bora zaidi na kuhakikisha wabunifu wanafanya ubunifu wenye tija utakaowaingizia kipato na taifa kunufaika.

"Serikali inahitaji kuona wabunifu wanasonga mbele katika kazi za ubunifu wanazofanya, ndiyo maana inawafuatilia kuendeleza kazi zao kupitia taasisi mbalimbali," alisema.

Akitoa mchanganuo wa wabunifu ambao ubunifu wao unaendelezwa, Dk. Akwilapo alisema 20 wako katika hatua nzuri, 85 wamefikia hatua ya kati huku 25 wakiwa katika hatua ya awali ya kuendelezwa.

Alisema lengo la serikali ni kuona vikundi vya ubunifu mbalimbali vinashawishiwa kwa kuendeleza ubunifu wa kazi zao ili wafike mbali na kulitangaza taifa.

Alifafanua zaidi ya kuwa tayari kumbi 17 mpya zimeanzishwa kwa ajili ya kuboresha kazi za wabunifu hao katika nyanja tofauti.

"Tunatarajia kutumia serikali za mitaa, SIDO na taasisi zingine kuhakikisha tunaendeleza kazi za wabunifu ikiwamo kuwatafutia masoko," alisema.




Habari na Augusta Njoji

## Serikali yaanika mkakati kutokomeza malaria

SERIKALI imejipanga kuhakikisha Mpango Mkakati wa Malaria (2021 – 2025) unapunguza kiwango cha malaria kutoka asilimia 7.5 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 3.5 mwaka 2025.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maida Hamad Abdallah.

Mbunge huyo alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali za kupambana na malaria, bado ugonjwa huo unaendelea kuwaathiri wananchi wakiwamo watoto.

"Je, serikali inaweza kutuambia hatua zilizofikiwa za kutokomeza ugonjwa huo?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikitekeleza afua na kazi mbalimbali za kudhibiti ugonjwa wa malaria nchini.

Alisema hatua hiyo imefanikiwa kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria kutoka zaidi ya asilimia 40 mwanzoni mwa miaka ya 2000 mpaka asilimia 7.5 mwaka 2017.

Alisema lengo mahususi la serikali ni kutokomeza kabisa ugonjwa wa malaria ifikapo mwaka 2030.

# Sheria ya Ndoa kufumuliwa

WIZARA ya Katiba na Sheria inaandaa muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa utakaowasilishwa bungeni, ili kuiboresha na kulinda makundi ya wanufaika na sheria hiyo.

Naibu Waziri, Geofrey Pinda, alibainisha hayo jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kurekebisha baadhi ya sheria kandamizi kwa wanawake ili ziendane na wakati.

Akijibu swali hilo, Pinda alisema serikali haina sheria kandamizi na kwamba sheria zote zinazotumika nchini zilitungwa na Bunge ambalo halijawahi kutunga sheria kandamizi.

Alisema serikali kwa kuzingatia mahitaji ya wakati na watu wake, imekuwa ikiwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuziboresha sheria hizo.

Hata hivyo, alisema kutokana na wakati uliopo na mahitaji ya sasa, serikali imeanzisha mchakato wa kuzipitia baadhi ya sheria ili zifanyiwe marekebisho kuendana na wakati.

"Hivi sasa, serikali kupitia wizara, imeandaa muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa utakaowasilishwa bungeni ili kuiboresha kwa lengo la kulinda makundi ya wanufaika na sheria hiyo," alisema.

Alisema serikali pia inaendelea na hatua mbalimbali za kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mirathi na Sheria za Kimila na hatua hizo zikikamilika, muswada wa mapendekezo ya kuzirekebisha sheria hizo utawasilishwa bungeni ili wabunge wapate nafasi nzuri ya kujadiliana na kuyapitisha marekebisho hayo.

Pia alisema wizara ipo katika mabadiliko makubwa ya kuhakikisha kunafanyika maboresho makubwa ya sheria ikiwamo kuzitafsiri kwa Kiswahili na kuweka vipengele kwenye sheria hizo vya kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili ili kuleta tija kubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Ninawaomba wabunge kuunga mkono juhudi za serikali katika eneo hili kwa lengo la kuimarisha utawala wa sheria na upatikanaji wa haki nchini," alisema.

Katika swali lake la nyongeza, Katimba alihoji kama serikali iko tayari kuanzisha divisheni ya familia ili ishughulikie masuala ya talaka na ndoa, kwa kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa.

Katika majibu yake, Pinda alisema ushauri huo ni mzuri na utafanyiwa kazi na mamlaka husika.

# Halmashauri zabanwa uzingatiaji miongozo

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imezitaka halmashauri za wilaya kufuata miongozo na taratibu za uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala unaohusisha uhitaji wa wananchi, viongozi wa wilaya na mkoa.

Imesema ipo tayari kupokea maombi ya kuanzisha maeneo mapya yasiyo na gharama na yaliyo karibu na wananchi.

Naibu Waziri Dk. Festo Dugange, alikumbusha kufuatwa kwa utaratibu huo alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, aliyetaka kujua ni lini serikali itaanza kutekeleza ahadi yake ya uongezaji maeneo ya utawala ambayo hayana gharama baada ya kusitisha kuyaongeza maeneo ya utawala yenye gharama.

Dk. Dugange alisema serikali ina dhamira ya dhati kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi na utaratibu wa kuomba maeneo hayo unafahamika.

"Nishauri pale ambapo kuna haja ya kusogeza maeneo hayo bila gharama, wahusika wafuate miongoni na taratibu kutoka TAMISEMI ili utaratibu ufanyike," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mlimba (CCM)m Godwin Kunambi, alitaka kujua lini serikali itaipa Mlimba hadhi ya kuwa wilaya hasa ikizingatiwa umbali mrefu wa takribani kilometa 200 ambao wananchi wanatembea kufuata huduma makao makuu ya wilaya.

"Ni lini serikali itaanza ujenzi wa majengo ya halmashauri na kuboresha miundombinu ya barabara?" Mbunge huyo alihoji.



Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Kenani, akiuliza swali bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Naibu waziri huyo akijibu swali hilo, alisema kwa mujibu wa miongozo na taratibu, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala unahusisha uhitaji wa wananchi, viongozi wa wilaya na mkoa ambao huwasilisha maombi ya mapendekezo yao kwenye Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na kisha kuwasilishwa TAMISEMI kwa hatua zaidi.

Alisema ofisi hiyo haijapokea maombi rasmi ya Mkoa wa Morogoro kuomba Mlimba kuwa wilaya.

"Serikali inashauri utaratibu huu uliowekwa ufuatwe. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba," alisema.

Alibainisha kuwa kwa upande wa miundombinu ya barabara, katika mwaka wa fedha 2019/20 serikali ilifanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 54, ilijenga kalvati 22 na madaraja manne kwa gharama ya Sh. milioni 545.87.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, serikali imetenga kiasi cha Sh. milioni 517.56 kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya barabara katika halmashauri hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi fainali zijazo za AFCON, CHAN yaanze sasa

**BAADA** ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kuondolewa mapema katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazokaribia ukingoni huko nchini Cameroon, huu ni wakati wa kuanza mapema maandalizi kwa ajili ya michuano ijayo.

Taifa Stars inayofundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije ilitolewa katika fainali hizo baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye kundi lake ikivuna pointi nne katika mechi tatu ilizocheza.

Stars ilianza kampeni za kuwania ubingwa wa michuano hiyo kwa kufungwa mabao 2-0 na Zambia halafu ikapata ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Namibia na kumaliza hatua ya makundi kwa sare ya mabao 2-2.

Timu hiyo pia ilishindwa kutoka mbele katika fainali za michuano hiyo zilizofanyika 2009 nchini Ivory Coast ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Marcio Maximo, ambaye ni raia wa Brazil kwa kumaliza na idadi ya pointi nne.

Kuteleza sio kuanguka, huu ndio wakati sahihi wa Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kukaa pamoja na kutathimini upungufu uliyojitokeza katika kikosi cha Stars kwenye fainali za CHAN mwaka huu na kuyafanyia kazi mapema.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia Stars kujiweka katika nafasi nzuri kwenye mechi za kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), badala ya kusubiri hapo baadaye.

Timu inapoandaliwa mapema, wachezaji wake huwa kwenye nafasi nzuri ya kuvuna matokeo chanya na hivyo kujiondoa katika nafasi ya kuonekana ni wasindikizaji kila inaposhiriki mashindano hayo makubwa kwa ngazi ya kimataifa.

Kikosi kinapopata maandalizi mazuri na kwa wakati unaostahili, inampa nafasi nzuri kocha kuwajenga wachezaji wake na kila mmoja kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha juu.

Nipashe inaikumbusha TFF kuongeza nguvu kwenye timu zake ili kupata ushindi katika kila mechi wanayocheza na kamwe kutowachukulia wachezaji wa Tanzania kama nyota wa mataifa mengine wanavyoyojiandaa.

Tunaamini kwa pande hizi mbili kukaa pamoja kutasaidia kupatikana muda mzuri wa kuwaandaa wachezaji kwa sababu baadhi ya nyota hao hawapati mazoezi ya kutosha wanapokuwa kwenye klabu zao.


Mazungumzo hayo yatasaidia kuwajenga wachezaji husika kwa maslahi ya nchi, lakini pia yatazisaidia klabu zao baada ya kurejea kutoka katika kambi ya Stars.

Inafahamika hakuna timu ya taifa au klabu yoyote inaweza kufanya vizuri katika mashindano yoyote inayoshiriki bila ya kujiandaa vyema, hakuna miujiza katika mchezo wowote hapa duniani, muhimu ni wachezaji kupata maandalizi yanayostahili.

Tunawakumbusha wahusika wote katika timu za taifa kuendelea kupambana kwa ajili ya kupata muda wa kutosha wa kuandaa vikosi vyao na hatimaye kwenda kwenye michuano kushindana na hatimaye kurejea na mataji au medali. Watanzania tusichoke wala Serikali na wadau wote tunatakiwa kutimiza majukumu yetu ipasavyo na ndani ya muda mfupi tutatimiza ndoto za kushinda mataji makubwa ambayo tumekuwa tukiyatamani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Nani anastahili kulaumiwa wachezaji kukosa mishahara?

**TAYARI** kuna dalili zote zinaonyesha baadhi ya klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara zimeanza kusuasusa kulipa mishahara wachezaji wao. Kuna taarifa mpaka sasa klabu nne za Ligi Kuu Tanzania Bara bado hazijawalipa mishahara wachezaji wake kwa muda wa miezi kadhaa mpaka sasa.

Licha ya viongozi wao wanaonekana kupiga chenga kujibu maswali hayo, badala yake kudai kila taasisi inadaiwa, kudaiwa ni suala ya kawaida, lakini ukweli unabaki pale pale kutolipa mishahara wachezaji ni kukiuka baadhi ya kanuni za Bodi la Ligi na mikataba waliyoingia na nyota hao.

Pamoja mambo mengi, Bodi ya Ligi inazitaka klabu zilipe mishahara wachezaji na kitendo cha kutolipa, ni kwenda kinyume cha kanuni.

Wakati ligi inaanza Bodi ya Ligi ilisema itakuwa wakali kusimamisha kanuni zake, lakini ifike wakati tu tuseme kwa mpira wa Tanzania kama ikitaka kufuata kanuni, basi zitabaki timu chache tu zenye uwezo wa kucheza ligi.

Na hizo zitacheza kwa sababu zina watu ambao wanazipa uwezo na si klabu zenye uwezo wa kujiingizia kipato.

Pamoja na kwamba soka la Tanzania kwa sasa ni la kulipwa, ambapo timu zote zinatakiwa ziwalipe mishahara wachezaji wake, tofauti na zamani ambapo zilikuwa ni za ridhaa tu, lakini ukweli unabaki pale pale, bado kuna dalili kuwa baadhi ya klabu bado zinajiendesha kiridhaa tu.

Nikisema soka la ridhaa, nina maana kuwa zamani wachezaji soka wakiwamo wa Simba na Yanga, walikuwa ni wafanyakazi wa mashirika au kampuni mbalimbali nchini Tanzania, na walifanya kazi na saa zao za ziada ndiyo walikwenda kuzichezea klabu zao.

Na huko walikuwa hawalipwi mishahara, bali posho za mazoezi, safari na bonasi pale wanaposhinda na zilitokana na viingilio vya milangoni.

Na hata mchezaji akiwa mikoani kama Tanga, Morogoro, Arusha, akitaka kusajiliwa na klabu labda za Dar es Salaam, Simba, Yanga, Sigara, Nyota Nyekundu na nyingine, moja na masharti ya usajili ilikuwa ni kutafutiwa kazi kwenye shirika au kampuni yoyote.

Kwa sasa haiko hivyo. Mpira sasa ni kazi kamili ambayo mchezaji anaishi kwa soka, hivyo anahitaji mshahara, marupurupu na mambo mengine.

Hapa nchini Tanzania kama ilivyo duniani kote tuko kwenye soka la kulipwa, lakini ukiangalia sana utakuta si la kulipwa moja kwa moja. Ni kama vile la nusu soka la kulipwa na nusu la ridhaa.

Wakati kuna klabu zikiwa zimesajili wachezaji kutoka nje ya nchi wakiwa wanalipwa mamilioni ya fedha, kuna baadhi ya klabu wachezaji wanalipwa posho tu na mshahara ni msamiati mpya kwao.

Zipo klabu ambazo zinalipa mishahara kwa kusuasua, yaani wachezaji wanaweza kukaa miezi mitatu wakalipwa mishahara wa mwezi mmoja kwanza, halafu wanasubiria tena. Wachezaji waishi kwa posho tu. Timu zote hizo zipo Ligi Kuu na zinacheza ligi moja.

Katika hili hajulikani hata wa kulaumiwa. Huwezi kuilaumu Bodi ya Ligi kwa kutochukua hatua, kwani kama ikitaka kuchukua hatua stahiki, inakachofanya ni kuziondoa timu ambazo zina matatizo ya kulipa wachezaji mishahara kwenye ligi. Ikifanya hivyo ligi itaharibika. Na hata ikitaka kufanya hivyo msimu ujao basi zitakazokuwa na uwezo huo ni timu chache, na tusishangae Tanzania ikawa ligi yenye timu ambazo hazizidi tano tu.

Bodi ya Ligi inajua matatizo ya klabu za Tanzania, ndiyo maana imekuwa ikienda nazo hivyo hivyo, ila ikizisisitizia tu ziepuke makosa hayo.

Ukisema uzilaumu klabu kwa kutolipa mishahara wachezaji, nako pia utakuwa unawaonea viongozi kwa sababu timu zinacheza soka kama burudani tu, hazizalishi au kuingiza chochote kile, hivyo ni ngumu kupata fedha za kuwalipa mishahara wachezaji wao.

# RC aonya wazazi ubakaji wa watoto

**Na Marco Maduhu,** HINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewaonya wazazi na walezi mkoani humo kuhusu tabia ya kulaza wageni kwenye vyumba vya watoto, akisisitiza kuwa kunachangia kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji.

Telack alitoa onyo hilo jana, wakati wa ufunguzi wa Asasi ya Wanawake Laki Moja mkoani Shinyanga ambayo imejikita kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii na kuinuana kiuchumi.

Alisema katika Mkoa wa Shinyanga, matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hasa wanayofanyiwa watoto ikiwamo mimba za utotoni na kubakwa, yanatokana na ndugu wa karibu na familia kwa kuwa wengi hulazwa chumba kimoja na wageni.

"Wazazi na walezi mkoani Shinyanga acheni tabia ya kulaza watoto wenu chumba kimoja na wageni, bali chukua watoto wako ulale nao, hicho chumba mwachie mgeni.

"Matukio mengi ya ukatili hasa ubakaji, yanafanywa na ndugu wa karibu. Pia toeni taarifa za matukio ya ukatili ambayo wanafanyiwa watoto wenu.

Pia mtoe taarifa za matukio mnayofanyiwa ninyi wenyewe, siyo kila siku unapokea vipigo, lakini husemi, mtaishia kuumia na hata kupoteza maisha," aliongeza.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo wa mkoa aliwataka wanawake mkoani humo, kuchangamkia fursa ya fedha za halmashauri asilimia 10 kwa kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali, ili wajikwamue kiuchumi na kuacha kuwa tegemezi.

Mwenyekiti wa Asasi ya Wanawake Laki Moja mkoani Shinyanga, Annaskolastika Ndagiwe, aliwataka wanawake waache kuficha wahalifu wa matukio ya ukatili na kutokwenda mahakamani kutoa ushahidi.

Alisema kupoteza ushahidi kunasababisha matukio hayo kuendelea kuwapo kutokana na watuhumiwa kutofungwa jela.

# Wanufaika TASAF waiangukia serikali

**Na Richard Makore,** MISUNGWI

BAADHI ya wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Misungwi mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuendelea kuwasaidia ili wajikwamue kutoka kwenye umaskini.

Wakizungumza na Nipashe wilayani Misungwi katika Kijiji cha Nyasato, wananchi hao walisema tangu walipoanza kupewa ruzuku kupitia mfuko huo, maisha yao yamebadilika.

Walibainisha kuwa mwaka 2015, familia nyingi ambazo sasa zinanufaika na mfuko huo, zilikuwa zikiishi maisha ya shida.

Mmoja wa wanufaika hao, Ester Lutende, alisema ruzuku ya TASAF imewasaidia kusomesha watoto kulima, kufuga mbuzi na kujenga nyumba bora.

Alisema kuwa baada ya kupata ruzuku hiyo, wanufaika walianzisha vikundi vya kusaidiana kupitia fedha hizo na kwamba mpango huo umezidi kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

Aliongeza kuwa kaya moja inapata kiasi cha kati ya Sh. 32,000 na 80,000 kwa mwezi na kwamba fedha hizo zimekuwa msaada kwao na kuipongeza serikali kwa kuendelea kuwasaidia tangu mwaka 2015.

Mratibu Msaidizi wa TASAF Wilaya ya Misungwi, Abigael Julius, alisema kuwa kati ya mwaka 2016 na 2019, wametumia zaidi ya Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya kusaidia kaya maskini.

Alisema fedha hizo zimetolewa na TASAF kwa wanufaika zaidi ya 5,000 katika Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza na kwamba wanahakikisha wanawasimamia na kuwatembelea ili kuona shughuli zao wanazofanya kuondokana na umaskini.

Alitaja baadhi ya mambo wanayofanya wananchi hao kupitia fedha za ruzuku kuwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, kusomesha watoto na kugharamia matibabu kupitia bima ya afya.

Sostenes Rwamkoba, Ofisa Kilimo Kata ya Mwaniko wilayani Misungwi, alisema ili kuhakikisha wananchi hao wanafanya kilimo cha kisasa, amepanga ratiba ya kuwatembelea na kuwapa ushauri.




Mratibu wa Ukimwi wa Manispaa ya Ubungo, Dk. Neema Mpanduji, akizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, baada ya kufunga kambi ya siku nne ya kupima magonjwa bure iliyoandaliwa na Hospitali ya Kairuki, eneo la Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mratibu wa Ukimwi abaini shida wananchi kupima afya

**Na Joseph Mwendapole**

MRATIBU wa Ukimwi Manispaa ya Ubungo, amewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kupima afya, ili kubaini maradhi yanayowasumbua mapema badala ya kusubiri kwenda hospitali pale hali inapokuwa mbaya.

Dk. Neema Mpanduji alitoa rai hiyo jana wakati akifunga kambi ya siku nne ya kupima afya iliyoandaliwa na Hospitali ya Kairuki maeneo ya Mbezi Luis jijini Dar es Salaam.

Mtaalamu huyo wa afya aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, alisema wataalamu wa afya wanawashauri wananchi kupima walau mara moja au mbili kwa mwaka badala ya kusubiri kwenda hospitali na vituo vya afya hali inapokuwa mbaya.

"Kuna magonjwa mengine hayaonyeshi dalili kama shinikizo la damu, sasa unapokuja hospitalini ukiwa umechelewa, unaweza kupata matatizo na wakati mwingine inabidi ulazwe. Kwa hiyo, tunahimiza mazoezi na kupima afya mara kwa mara," alisema.

Alisema kwenye hospitali zote, uchunguzi wa saratani ya shingo ya mlango wa kizazi na ya matiti umekuwa ukifanyika bila malipo, hivyo hakuna sababu wananchi kutokwenda kupima afya ili kujua hali zao.

"Ninawahimiza wanawake wakapime saratani hii na ya matiti, ninawahimiza wananchi na walezi wenye watoto wa kike chini ya miaka 14 waende wakapate chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi ambayo inatolewa bure kwenye hospitali zote za binafsi na za serikali," alisema.

Kaimu Meneja Uhusiano na Masoko wa Hospitali hiyo, Arafa Juba, alisema kambi hiyo hufanyika kila mwaka kwa ajili ya kumwenzi mwanzilishi wa hospitali hiyo, Hayati Profesa Hubert Kairuki.

Alisema mbali na kupimwa, wananchi wanaofika kwenye kambi hiyo wamekuwa wakipata ushauri wa kitabibu kutoka kwa madaktari wa hospitali hiyo wa namna ya kwenda kutibu maradhi yanayowasumbua.

"Tunawapima pia wenye uoni hafifu na kwa wale wanaohitaji miwani, tunawapa miwani bure. Pia tumefanikiwa kuhamasisha wananchi wengi wajiunge na bima ya afya iliyoboreshwa," alisema.

Alisema Hayati Profesa Kairuki aliyefariki Februari 6 mwaka 1999, mbali na kuwa mwanzilishi wa hospitali hiyo, pia ni mwanzilishi wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) na Shule Kuu ya Uuguzi ya Kairuki.

Arafa alisema Profesa Kairuki pia ni mwanzilishi wa Mtandao wa Shirika la Afya na Elimu (KHEN) na kiwanda cha kutengeneza dawa cha Kairuki Pharmaceuticals Industry kilichoko Zegereni, Kibaha.

MAKALA DODOMA

# TARURA inavyozisuka barabara Dodoma

Na Mwandishi Wetu,
DODOMA

MKOA wa Dodoma ambao ni Makao Makuu ya nchi, umeanza kupambwa kwa kuwa na barabara za lami kuanzia Dodoma Mjini na kwenye wilaya zake ili kuupa mkoa huo hadhi yake tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma, barabara nyingi hazikuwa katika hali nzuri.

Pamoja na barabara, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), unafanya matengenezo na maboresho ya madaraja ili kuwezesha shughuli za usafirishaji kuwa rahisi.

Miundombinu ya barabara pamoja na madaraja kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mvua hasa pale mvua inaponyesha kupita kiasi kwa muda mrefu, mfano mvua zilizonyesha kwa mwaka wa fedha 2019/20 zilichangia kwa kiasi kikubwa kuharibu madaraja na barabara katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, mvua hizo zilisababisha kuharibika kwa daraja lililopo Mto Bubu, Kata ya Thawi katika barabara ya Changaa - Thawi yenye urefu wa Km 14.9.

Kuharibika kwa daraja hilo kulisababisha kero kubwa kwa wananchi ambao walishindwa kwenda hospitalini pamoja na shuleni baada ya mawasiliano kukatika kutokana na mvua hizo, TARURA ilitenga Sh. milioni 383 ili kurejesha mawasiliano.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Mhandisi Brighton Kimaro ambaye ni Meneja wa TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, anaeleza kuwa fedha hizo zilitolewa na kazi kuanza ambapo hadi sasa matengenezo yamekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wanatumia daraja hilo kwa shughuli zao ambapo huduma kama elimu na afya zinafikika kwa urahisi.

"Eneo hili la daraja upande wa kuingilia lilikatika na kusababisha kukatika kwa mawasiliano, tulifanya jitihada kwa kuomba fedha za kazi hiyo ya kurejesha mawasiliano na kuanza kujenga kuta za mawe (Gabions), ujenzi huu umegharimu Sh. milioni 383 na kingo zote mbili za daraja zimekamilika," anasema Mhandisi Brighton.

Juma Hapi ni Diwani wa Kata ya Thawi, ambaye anelezea kuwa TARURA imetimiza vizuri wajibu wake wakuwezesha wananchi katika shughuli za usafiri na usafirishaji kwa urahisi kwani baada ya mawasiliano kukatika hawakutarajia kama yangerejeshwa kwa muda mfupi na hili linatokana na hali ya Mto Bubu kuwa na maji mengi, aliongeza kuwa daraja hilo ni kiunganishi kikubwa kati ya kata ya Changaa pamoja na Kata ya Thawi.

Diwani anaeleza kuwa daraja lilipokatika lilileta adha kwa wananchi kwa kukatisha mawasiliano baina ya kata mbili na kusimamisha huduma za kijamii hivyo kusababisha kukosekana kwa huduma kama shule pamoja na wagonjwa kushindwa kwenda hospitalini.

"Hakuna mtu aliyetarajia kwamba eneo hili litapitika tena, lakini tunawapongeza TARURA kwa kurejesha mawasiliano katika eneo hili kwa kushirikiana na wananchi kuweza kurudisha mawasiliano katika kata zetu hizi mbili maana huduma zote zimerejea kama hapo awali," anasema diwani.

Mbali na urejeshaji wa mawasiliano TARURA imetekeleza ujenzi wa barabara za lami zenye jumla ya urefu wa kilomita sita ambazo zimebadilisha maeneo ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa na kuondoa kero za muda mrefu kwa wakazi wa mji huo.

Kwa upande wa Wilaya ya Chemba, TARURA imeendelea kufanya matengenezo ya barabara ya Chandama - Soya - Mwakivabe yenye urefu wa kilomita 31.2, barabara hiyo ni kiungo muhimu kwa wananchi kwa kuwarahisishia shughuli za usafiri na usafirishaji ili kuwawezesha kwenda Chamwino pamoja na kwenda katika maeneo ya jirani ambapo siku za nyuma ilikuwa haipitiki hasa katika kipindi cha mvua, lakini baada ya TARURA kuanza matengenezo ya mara kwa mara hasa katika maeneo korofi sasa inapitika kwa vipindi vyote.

Naye Meneja wa TARURA katika Halmashauri ya Chemba, Mhandisi Mathias Makaju, anaeleza kuwa mbali na matengenezo ya barabara hiyo, eneo korofi ambalo lilikuwa linakwamisha shughuli zote kwa kukatisha kwa mawasiliano ni katika eneo la Kata ya Soya, ambapo ujenzi wa kalavati ulifanyika ili kuunganisha kata tatu ambazo ni Kata ya Kimaha, Kata ya Soya pamoja na Kata ya Msaada kwa gharama za Sh. milioni 90 ili kuwaondolea kero za muda mrefu kwa wakazi wa Chemba.

"Barabara ya Chandama - Soya - Mwakivabe ina urefu wa kilomita 31.2 imekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa Wilaya ya Chemba, pia daraja hili ni muhimu kwa wananchi wa Chemba, tumeamua kufanya hivi ili tuwawezeshe wananchi kuvuka kutoka eneo moja kwenda jingine na kuwawezesha kusafirisha mazao yao kama alizeti, mahindi pamoja na kuwezesha shughuli kubwa za mnada mkubwa ambao huwa unafanyika katika maeneo hayo," anasema.

Mashaka Rajabu ambaye ni mkazi wa Kata ya Soya anaeleza kuwa wananchi ni mashuhuda wa kazi za TARURA kwani wanatumia barabara hiyo katika vipindi vyote vya mwaka kwani ilikuwa ni shida kwenda mjini kwani barabara zilikuwa hazipitiki kabisa, lakini kwa sasa wanaipongeza TARURA kwa kuwaunganishia Kata hizo tatu pamoja na Wilaya Chamwino na Kiteto na kuwezesha mnada kufanyika kwa urahisi.

TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ipo katika ujenzi wa Daraja la Miembeni ambalo litaondoa kero ya kukatika kwa mawasiliano katika Mji wa Mpwapwa hasa katika kipindi cha mvua kwani daraja hilo lenye urefu wa mita 25 litagharimu Sh. milioni 900 hadi kukamilika kwake na linajengwa chini ya Mkandarasi Technics Construction Group Ltd ambaye ameeleza kuwa ujenzi wa daraja hilo umefikia asilimia 50 ili kukamilika, mradi huo pia unatekelezwa baada ya daraja la awali lenye urefu wa mita 10 kusombwa na maji kwa zaidi ya mara mbili na hivyo kusababisha kukatika kwa mawasiliano ndani ya mji huo.



Mwonekano wa ujenzi wa daraja la Miembeni lenye urefu wa mita 25 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma. **PICHA: TARURA**

Mhandisi Emmanuel Lukumay ambaye ni Meneja wa TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa anaeleza kuwa hadi sasa Mji wa Mpwapwa una kilomita tatu za lami, lakini ujenzi wa wa daraja la Miembeni unaendelea kuunganisha mji huo.

"Ujenzi wa daraja la Miembeni lenye urefu wa mita 25 umefikia asilimia 50 na utagharimu Sh. milioni 900, pia mpaka sasa katika Wilaya yetu ya Mpwapwa tumetekeleza Kilomita 10 za lami ya zege ambazo zipo milimani," anasema Mhandisi Lukumay.

Samwel Mapuga ambaye ni Mkazi wa Mpwapwa anaeleza kuwa kabla ya TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa haina lami, lakini kwa sasa wanaona jitihada za TARURA katika kuhakikisha Wilaya ya Mpwapwa inakuwa na lami na kuwawezesha kufanya shughuli zao za usafiri na usafirishaji katika kipindi chote cha mwaka, aliongeza kuwa baada ya TARURA kuanzishwa, sasa hatua zinachukulia kwa haraka hasa pale mawasiliano yanapokatika.

"Unaweza kujionea mwenyewe kuwa uwepo wa TARURA katika halmashauri yetu ya Mpwapwa sasa ina barabara za lami na hatukuwahi kutarajia, lakini ujenzi wa daraja hili kubwa ni chachu ya maendeleo yetu," anasema Mapuga.

Kwa upande wake, Mratibu wa TARURA Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, anaeleza kuwa uboreshaji wa barabara za Dodoma Mjini unaendelea huku akitolea mfano eneo la Kisasa maarufu kama Nyumba 300 - FFU tayari mkandarasi amepatikana ili kuanza ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 1.0 kwa kiwango cha lami na kuongeza kuwa matengenezo na maboresho ya miundombinu yanaendelea katika maeneo mbalimbali ya Jiji.

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), mkoani Dodoma una mtandao wa barabara wenye jumla ya urefu wa kilomita 6,996.25 ambapo lami na zege ni kilomita 179.70, brabara za changarawe 1034.198, na barabara za udongo 5,782.352.

TARURA imeendelea kujikita katika kuwezesha wananchi kupata huduma ya usafiri na usafirishaji kwa urahisi kwa kutengeneza na kuboresha barabara vijijini na mijini ikiwa ni pamoja na makalavati, madaraja na mifereji ya maji.





# Mbunge alia na bei za pembejeo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameiomba serikali kuwa na mkakati maalum wa kuhakikisha pembejeo zinazotumika kwenye zao la korosho zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu.

Akichangia juzi hoja ya hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa bungeni Novemba 13 mwaka jana wakati akifungua rasmi Bunge la 12, Chikota alisema Rais katika hotuba yake hiyo alibainisha namna kilimo kinavyopaswa kuwa cha kibiashara na kuahidi upatikanaji wa pembejeo na viatilifu kwa wakati na kwa bei nafuu.

"Sisi Mtwara zao kuu la uchumi ni korosho. Ninaomba serikali kuwa na mkakati maalum wa kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu.

"Tuhakikishe zao la korosho tunapanua soko lake, kuna minada inayoendelea lakini kuna TMX (Soko la Bidhaa Tanzania), sasa hivi wanashiriki wanunuzi wale wale wanaoingia minadani, hebu TMX iwezeshe ili tuwapate wanunuzi wakubwa kutoka Vietnam na China.

"Wasitumike wanunuzi tunaowaona kwenye minada, tuwe na tofauti kwenye TMX, tuwe na wanunuzi wakubwa, huku kwenye minada tubaki na wanunuzi ambao huwa tupo nao," alishauri.

Mbunge huyo alisema kuna haja serikali ijielekeze katika kuwawezesha wabanguaji wadogo ili waongeze thamani kwenye korosho badala ya kuuza korosho ghafi.

Kuhusu miundombinu, Chikota aliomba serikali kutafuta chanzo kingine cha fedha ili kuuongezea fedha Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), ili ufanye kazi yake kwa ufanisi.

"Niipongeze kamati yetu ya ulinzi na usalama kwa kufanya kazi nzuri kwenye mpaka wa Tunduma, sasa ninaomba barabara hii ya ulinzi ijengwe kwa kiwango cha lami, kutoka Mtwara hadi Mbinga. Ni barabara muhimu kwa ulinzi na usalama wa nchi," alisema.

Vilevile, aliomba serikali iweke kiwango maalum cha tozo kwa meli zinazoingia Mtwara, ili kuwavutia wenye meli kupeleka meli nyingi kwa wakati huu.

"Ukiifanya Bandari ya Dar es Salaam na Mtwara kuwa na 'rate' sawa hii, haitawavutia kupeleka meli Mtwara, ninaomba kuwe na kiwango maalum ili kuwavutia wawekezaji kuleta meli Mtwara," alishauri.

# Sababu wanaume wenye VVU kufa mapema kuliko wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAUME wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) wanaongoza kwa kupoteza maisha nchini kutokana na kutoanza mapema kutumia dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo pindi wanapobainika wana maambukizi kulinganishwa na wanawake.

Akizungumza jana katika kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi na Dawa za Kulevya, Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema takwimu za maambukizi mapya zinaonyesha yapo mengi kwa wanawake kuliko kwa wanaume.

"Inapokuja suala la upimaji, wanaume wanakuwa nyuma na hii siyo tu nyuma katika kupima, lakini pia hata ukiwafuatilia wale waliopima, wapo nyuma kuanza dawa kwa sababu kusudi la kupima ni ili mtu aingizwe kwenye dawa," alisema.

Alibainisha kuwa idadi yao inapungua kutokana na kutoanza dawa mapema baada ya kubainika wana maambukizi.

"Pia, hata wakianza dawa wanaume wapo nyuma kufubaza VVU, hawatumii dawa vizuri, kwa maana ya ARVs, ndiyo wanaongoza kwa vifo vingi kulinganisha na wanawake ambao wao wanapima haraka, wanaanza dawa haraka na wanazingatia kutumia dawa ndiyo maana hawafariki haraka,"alisema.

Alifafanua kuwa takwimu za mwaka 2019, zinaonyesha watu wazima na watoto wanaoishi na VVU ni milioni 1.7, wanaume wakiwa 628,830 na wanawake 983,471.

Alisema vifo vinavyotokana na ugonjwa huo kwa wanaume ni 12,225 kulinganishwa na wanawake 9,304.

"Maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka 2019 ni 77,084 ambapo wanawake ni 39,614 na wanawaume ni 28,870 huku watoto chini ya miaka mitano ni 8,600," alibainisha.

Alisema hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuhamasisha wanaume kupima na kuanza matumizi ya dawa.

Mbunge wa Maswa, Stanslaus Nyongo, alisema kutokana na hali hiyo, kamati inapaswa kushughulikia suala hilo kwa kuhakikisha watu wanapima na kuanza dawa mapema na kuendelea kutumia dawa hizo.

Awali, akifungua kikao hicho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Watu Wenye ulemavu, Jenista Mhagama, alisema huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU zimeimarika nchini.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 2019, zaidi ya watu milioni 1.2 walikuwa wanapata huduma ya dawa.

Mhagama alisema mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuimarika kwa huduma ya upimaji wa VVU na utoaji wa elimu hasa kwa vijana kutokana na kundi hilo kuonekana kuongoza kwa maambukizi mapya.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Mbunge wa Same Magharibi, Dk. David Mathayo (katikati) na Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM.**

# Wanawake wapewa mbinu kukabili kansa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), amewataka wanawake kujenga tabia ya kupima afya zao mara kwa mara, ili kujikinga na magonjwa ya saratani ya matiti na shingo ya uzazi ambayo yanatibika.

Gaudensia Kabaka alitoa rai hiyo wakati wa maadhimisho ya miaka 44 ya kuzaliwa kwa chama hicho jijini Dodoma jana.

Alisema kila mwanamke anapaswa kujiwekea utaratibu wa kupima afya yake badala ya kusubiri mpaka aumwe ndiyo aende hospitali, akisisitiza jambo hilo siyo sahihi kwa afya ya binadamu.

"Wanawake tunapaswa kujenga utaratibu wa kupima afya kuangalia magonjwa ya saratani ya matiti na shingo ya kizazi ambayo husumbua. Tukifanya hivyo, itatusaidia kuyatokomeza," alisema.

Kabaka alisema lengo lao ni kuona wanawake wote wanakuwa mstari wa mbele kuhimiza wanawake wengine kwenda kupima afya zao.

Mbali na hilo aliwataka UWT kuanzisha miradi mbalimbali ambayo itawasaidia kujiendesha wenyewe badala ya kuwa ombaomba.

Kabaka alisema serikali ya sasa inafanya vitu kwa kujitegemea, hivyo wao kama UWT wanapaswa kuwa na vitega uchumi vyao, ambavyo vitawasaidia kujiendesha.

"Tujipange kuwa na miradi mbalimbali ambayo itatuingizia kipato, tuna kila sababu ya kufanya hivyo kwa sababu uwezo tunao," alisema Kabaka.

Alisema UWT ikiwa na miradi kila mkoa, itasaidia kwa kiasi kikubwa kufanya mambo mbalimbali ya msingi ambayo yatajenga.

Aliwapongeza UWT mkoani hapa kutokana kuazimisha miaka 44 ya kuzaliwa CCM kwa kutoa misaada katika vituo vya watoto yatima, hospitalini na kufanya usafi katika maeneo mbalimbali.

Kabaka alisema UWT wanapaswa kuendelea na moyo huo, siyo mpaka wakati wa sherehe ndiyo watoe msaada

Alisema wanawake ni jeshi kubwa na wakiamua kufanya jambo lolote, wanaweza kwa sababu wakianzisha, wanakuwa wamekusudia.

Alisema kinachotakiwa ni ushirikiano wa kila jambo wanalofanya kuhakikisha linaleta matokeo chanya.





# Rais apongeza utendaji Uhamiaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, ameipongeza Idara ya Uhamiaji kwa kutekeleza vyema majukumu yake na kuanza kutafuta ufumbuzi wa tatizo la foleni kwa wageni ndani ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Dk. Hussein Ali Mwinyi alitoa pongezi hizo jana alipozungumza na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Peter Makakala, aliyefika Ikulu Zanzibar, kwa ajili ya kujitambulisha.

Rais aliipongeza idara hiyo kwa kuanza kuyafanyia kazi matatizo yaliyopo katika uwanja huo, akiamini hatua hizo zitapunguza foleni kwa wasafiri wakiwamo wageni ili wawe wanarudi tena kuitembelea Zanzibar.

Alisema tatizo la foleni lilikuwa likiwasumbua wasafiri wakiwamo wageni hasa ikizingatiwa kwamba uwanja huo ni lango la watalii kutoka nje ya nchi, hivyo ufumbuzi utasaidia kukuza Sekta ya Utalii.

Aliongeza kuwa juhudi za makusudi zitachukuliwa katika kuhakikisha jengo jipya la uwanja wa ndege litakapoanza kazi matatizo kama hayo hayajitokezi.

Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuupongeza uongozi wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa kuyafanyia kazi matatizo na kuongeza madawati katika uwanja huo wa ndege.


Aliitaka idara hiyo kuhakikisha kila mgeni anayekuja, awe ameshapata VIZA yake ili kuepuka kukaa foleni muda mrefu katika uwanja huo.

Pia, alisema kuna haja kulitafuatia ufumbuzi tatizo la mfumo wa uhamiaji kuwa chini na kupelekea kuchelewa kwa wageni na kusababisha foleni.

Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Makakala, alimpongeza Dk. Mwinyi, akisema kazi za idara hiyo zitaendelea kuimarishwa kwa weledi na kutoa ushirikiano.

Alisema idara hiyo imeimarisha mifumo ya utoaji wa huduma na kuimarisha mfumo wa uhamiaji mtandao ambapo tayari wameshaanza kutoa pasi za kusafiria za elektroniki.

Alisema idara hiyo inatoa VIZA kwenye mitandao, vibali vya ukaazi pamoja na udhibiti wa mipaka ambapo hatua hiyo imeweza kuimarisha mapato kwa kiasi kikubwa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiagana na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Peter Makakala (wa pili kulia) baada ya kumalizia mazungumzo, Ikulu Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU.**

# Mkandarasi matatani jengo lililoporomoka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhamed Mussa, amesema wizara itamchukulia hatua za kisheria mkandarasi aliyejenga Jumba la Bet al Ajab na kusababisha kuporomoka kwa jengo hilo.

Amesema hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kumtaka kulipia fidia ya uharibifu wa mali uliojitokeza.

Waziri huyo amesema mbali na fidia hiyo, pia kupitia Sheria ya Madai, wizara itahakikisha mkandarasi huyo analipia fidia ya afya na uhai wa watu walioathirika katika tukio hilo.

Lela alitoa kauli hiyo juzi wizarani kwake Kikwajuni mjini Unguja, alipotoa ripoti ya Kamati ya Uchunguzi ya Kuporomoka kwa jengo hilo Desemba 25 mwaka jana.

Alisema mbali ya hatua hiyo, wizara pia itawawajibisha kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma watendaji wakuu waliokuwa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mamlaka ya Hifadhi na Undelezaji wa Mji Mkongwe, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati.

Alisema wizara pia inashauri mamlaka ya uteuzi kuivunja bodi na kuunda bodi mpya, kufanyiwa marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi ya Uendelezaji wa Mji Mkongwe hasa katika maeneo ya sifa ya wajumbe wa bodi.

"Tutachukua hatua za kuvunja timu ya usimamizi ya mradi na kuajiri mshauri elekezi mwenye sifa na weledi wa kusimamia mradi kama huo," alisema.

Alisema Mshauri Elekezi wa mradi huo atachukuliwa hatua za kimkataba pamoja na wahusika wengine ambao watawajibishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) na kuwataka wahusika warejeshe fedha zote kwa umoja wao.

Alisema hatua hiyo imekuja baada ya kubainika kasoro mbalimbali katika mradi huo wa ujenzi wa jengo la Bet al Ajab ambalo liliporoka mwishoni mwa mwaka jana.

Waziri Lela alitaja baadhi ya kasoro hizo kuwa ni Mshauri Elekezi kujipatia Sh. milioni 58.700 na kwamba licha ya mkandarasi kushindwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa mkataba waliopewa, alilipwa Sh. milioni 86.8 kinyume cha taratibu za kisheria.

Alisema kasoro nyingine ni wizara kushindwa kusimamia timu ya usimamizi wa mradi katika utekelezaji wa mkataba na Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kushindwa kusimamia utekelezaji wa ujenzi huo.

Alisema kasoro nyingine ni kubainika kuwasilisha na kuthibitisha bima yenye utata juu ya kulipia fidia za hasara iliyojitokeza pamoja na kushindwa kutekeleza majukumu ya mkataba kwa mujibu wa masharti ya mkataba.

Waziri Lela alisema mradi wa jengo hilo ulianza Novemba mwaka 2019 na kutarajiwa kukamilika Februari mwaka huu, ukipangwa kutumia Dola 5,931,770.7 ambazo ni ufadhili wa Serikali ya Oman.

## SMZ kushirikiana na asasi za kiraia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imesema itaendelea kushirikiana na asasi za kiraia ili kuchochea kasi ya mabadiliko na maendeleo ya jamii.

Mkurugenzi wa Asasi za Kiraia kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Ahmed Khalid Abdulla, aliyasema hayo jana alipofungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi wa mradi wa kuziwezesha asasi za kiraia kutumia vyombo vya habari yaliyoandaliwa na Zanzibar Youth Forum (ZYF).

Alisema asasi za kiraia zina jukumu la kushirikiana na serikali katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii, hivyo kuna umuhimu wa pande mbili hizo kufanya kazi kwa kushirikiana.

Aliipongeza jumuiya hiyo kwa kufikiria kuwajengea uwezo vijana juu ya matumizi ya vyombo vya habari hasa vya kijamii ili kuepuka migogoro ndani ya jamii.

"Wazo la kuwajengea uwezo wadau wenu ni muhimu na litapunguza migongano ya kijamii kutokana na makosa yanayofanyika hasa mitandaoni," alisifu.

Alizitaka asasi za kiraia kutofanya kazi kimya kimya badala yake zishirikiane na vyombo vya habari katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Vyombo vya habari ni muhimu katika kutangaza shughuli zenu na kunufaisha sehemu kubwa ya jamii, hivyo ninawaomba mvitumie, msifanye kazi kimya," alishauri.

Awali akitoa maelezo ya mradi huo, Mkurugenzi wa ZYF, Maulid Suleiman Juma, alisema mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la International Media Support (IMS) la Denmark, umelenga kutambua matatizo yanazoikabili jamii juu ya matumizi ya vyombo vya habari.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo, kwa kipindi cha miaka mitatu, wadau mbalimbali watahusishwa ili kuwasaidia vijana kukuza na kutumia vyema uhuru na upatikanaji wa habari.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Faki Khamis Faki, alisema ZYF ina wajibu wa kushughulikia matatizo yanayowakabili vijana yakiwamo makosa ya mitandao.



**ZUCHU**

UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



SIKU Chache baada ya Diamond Platnumz, kukiri hadharani kwamba mzee Abdul sio baba yake na kumtaja Salum Nyange kuwa mzazi wake halisi, msanii huyo amejikuta akipata balaa zito katika kazi yake ya muziki.

Wakati mgogoro huo ukiendelea kutikisa, Diamond alikuwa akijifua vikali kwa ajili ya kwenda kutumbuiza katika sherehe za utoaji tuzo za muziki wa Afrika, maarufu kama 'MTV Africa Music Awards (MAMAs).

Hata hivyo, jana waandaaji wa tuzo hizo wametoa tangazo la kufuta sherehe hizo ambazo zimepangwa kufanyika katika jiji la Kampala nchini Uganda mwezi huu.

Kupitia ukurasa wa Twitter, bila kutoa sababu MTV Base Africa, imesema tuzo hizo hazitafanyika mwaka huu na taratibu za kuwatangazia watu zinaendelea.

Awali Diamond, alisikika akisema kwamba anataka kwenda kuonyesha maajabu katika tuzo hizo ambazo yeye alichaguliwa kutumbuiza.

Kufutwa kwake itakuwa pigo la kwanza kwa mwanamuziki huyo tangu kuwapo malumbano kati ya familia mbili ya Mzee Abdul na mama yake Diamond, kuhusu nani baba yake halali.

Hivi karibuni, tuzo hizo zimekuwa zikipigwa vita na wanaomuunga mkono Bobi Wine, Jeffrey Smith na Robert Amsterdam, wakitaka waandaaji kufikiria tena kuhusu kufanya tamasha hilo nchini Uganda.

"Sio tu kwamba litakuwa linafuta uhalifu uliofanywa na utawala huo, lakini pia litaathiri wasanii wote walioteuliwa," Jeffrey Smith aliandika ujumbe kupitia Twitter.

Tamasha hilo maarufu lilitakiwa kuendeshwa mubashara kupitia mtandaoni kutokana na janga la virusi vya corona.

Tuzo hizo ambazo mara ya kwanza zilifanyika 2008, Afrika Kusini mwaka 2016 na 2009 zilifanyika nchini Kenya.

## MWAKA MBAYA

# Diamond apata balaa la kwanza

BASI SAWA

## Zuchu katika rekodi nyingine

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Zuchu, amezidi kuweka historia baada ya kuvunja rekodi nyingine kwa kuwa mwanamuziki wa kwanza wa kike kutoka Afrika Mashariki kwa kufikisha watazamaji milioni mia moja kwenye akaunti yake YouTube.




Zuchu anaongoza akiwa idadi kamili ya watu waliotazama 103,202,342 na akifuatiwa na Nady ambaye amepata watazamaji 91,568,549, kisha nafasi ya tatu imemuangukia Vanesa Mdee mwenye 38,666,916.

Hata hivyo, Nadi Mukami kutoka Kenya ameshika nafasi ya nne akiwa na 33,234,293 na Tanasha Donna akiwa na 20,303,429.

## Lady Jaydee apigiwe makofi

MSANII kongwe wa muziki, Lady Jaydee, anayejulikana pia kama Komando Jide, amesema muziki wa sasa unawahi kupotea kwenye masikio ya watu kama ilivyo 'Bubble gum' inayotafunwa na kutemwa.



Akizungumza katika kipindi cha Friday Night Live cha East Africa Television (EATV, amesema hayo baada ya kuulizwa kwanini muziki wa zamani unaishi mpaka sasa na muziki wa kizazi kipya unapotea haraka.

"Wasanii wa siku hizi wanafanya 'bubble gum music' unakuwa ni muziki wa muda mfupi tu ili uwalipe kwa hapo hapo lakini 'in a long run' hakuna muziki", amesema.



## Harmonize ataja sababu Ibrah kukwama

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Harmonize, amezungumzia sababu ya msanii wake Ibrah Tz, kushindwa kuingiza nyimbo zake katika mtandao wa You Tube.

Kupitia ukurasa wake wa Istagram, Harmonize, amesema msanii wake huyo amekumbana na changamoto ya kazi zake kutoingia katika mtandao huo na juhudi zinafanyika kurekebisha.

" Chinga amekumbana na changamoto kupitia mtandao wa you tube kazi zake kutoingia kwenye trend, lakini ilishatokea hata channel yake kufutwa kabisa uongozi wake ukapambana na kuirudisha. Kwa niaba yake niwashukuru wote mlionae bega kwa bega na kuamini katika kipaji chake na kumpa nguvu zaidi," amesema Harmonize.

## Unyago: Mchawi binadamu, paka katumwa tu

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE baadhi ya jamii za Kiafrika huamini mnyama paka akilia usiku, basi ni dalili za uchawi. Baadhi humuogopa wanyama hao, hasa wale wanaoonekana usiku.

Hata hivyo, kutokana na imani hizo, wengine wakaenda mbali na kuja na msemo kuwa hata kama paka ana ishara au dalili za uchawi, lakini mbaya atakuwa ni binadamu tu na si mnyama huyo kwa sababu atakuwa ametumwa tu kufanya hivyo.

Ina maana binadamu ndiye ametumia njia ya kupandikiza paka huyo kwa ajili ya kujificha yeye asionekane tu. Ndipo wakaja na msemo huu wa 'Mchawi binadamu, paka katumwa tu."

Msemo huu unaakisi kile kilichomo kwenye filamu ya 'Unyago.' Ni filamu inayoonyesha kuwa wakati mwingine mtu anaweza kupata matatizo, mikosi na majanga kibao, lakini chanzo ni watu wa karibu wanaokuzunguka.

Filamu inaanza ikionyesha kuwa mama Batuli anataka binti yake Batuli achezwe unyago, lakini baba mtu  HYPERLINK "http://anakataa.na" \t "_blank" anakataa na kusema ni



mila zilizopitwa na wakati.

Upande wa pili, kijana mmoja anaitwa Tuga anampenda Batuli. Lakini kuna msichana Sikitu ambaye ni binti wa shangazi wa Batuli, naye anampenda Tuga.

Kinachotokea ni kwamba mama Tuga na mama Sikitu, wanafanya kila njia kuhakikisha Tuga anafunga ndoa na Sikitu na si Batuli.

Hata barua ya posa ilipopelekwa kwa kina Batuli, shangazi mtu hakumaliza hata hafla ya upokeaji barua hiyo, akaondoka. Akaenda hadi kwa mama Tuga kumweleza kuwa mwanaye amekwenda kutoa barua ya uchumba kwa kina Batuli badala kuleta kwa binti yake Sikitu.

Wote wanakasirika na kwenda kwa mganga kwa lengo la kumdhuru Batuli. Na kweli siku ya kutolewa, mwali anaanguka chini na kuzimia na sherehe zote zinavunjika. Anatibiwa anapona.

Lakini hiyo haimfanyi Tuga kuahirisha lengo lake la kumuoa Batuli. Anamuona kwa lazima. Harusi imekwisha, mama mkwe hamtaki mke wa kijana yake. Chaguo lake lilikuwa ni Sikitu.

Kutokana na hali kuwa mbaya nyumbani, kwani Tuga alikuwa bado anaishi kwa wazazi wake, akaanza ulevi ili kuondoa mawazo ya mama yake ambaye kila kukicha alikuwa akimtukana binti wa watu.

Ulevi ukasababisha na yeye awe anampiga mkewe. Mke akaona arudi kwao. Huku nyuma, rafiki zake wakamkalisha chini Tuga na kumshauri amrudie mkewe na aache ulevi. Anafanya hivyo. Anaacha pombe, anarudiana na mkewe na kuamua kuondoka nyumba kwa mama yake, kwenda kuanza maisha mapya mbali na kijiji hicho akiwa na mkewe Batuli.





## Nuh Mziwanda, Aslay washirikiana 'Kanitodokoa'

WANAMUZIKI wakali katika muziki wa Bongo Fleva, Aslay na Nuh Mziwanda, hatimaye wametambulisha kazi yao mpya inayoita 'Kanidokoa'.

Wasanii hao ambao kwa mara ya kwanza wameshirikiana kuimba, wameweka kazi hiyo katika mtandao wa You Tube.

"Mashabiki wetu watapata ladha tofauti kutoka kwetu, hii ni kazi nzuri kwa mwaka 2021," amesema Nuh.

## WIVU NI KINGA YA MAPENZI AU KERO?

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE mapenzi kuna kitu kimoja kinaitwa wivu. Ni hali ya kutotaka mpenzi, mume au mke asiwe na mtu mwingine yoyote zaidi yako.

Hali hii huja yenyewe tu kwa viumbe wengi na binadamu hasa pale anapommiliki ampendaye. Hakuna mtu anayemuonea wivu mtu ambaye hayuko naye, au hajaanza naye uhusiano. Lakini ukishaanza na hali hiyo nayo inajitokeza.

Pamoja na hayo, bado hadi leo hakuna anayeweza kufafanua vizuri kuwa wivu kweli ni kinga ya mapenzi, au huwa kero kwa wapendanao.

Leo tunaziangalia nyimbo za dansi ambazo wanamuziki waliimba kuhusu wivu. Ni kitu gani? Kinasababishwa na nini? Dawa yake nini?

**Wivu-Vijana Jazz Band**

Wimbo huu wa miaka ya mwishoni mwa 1980 ni utunzi wake marehemu Eddy Sheggy. Unaitwa 'Wivu'. Mwanamke anauliza kama kuna hospitali ya wivu ipo duniani ili akatibiwe. Tatizo ni kwamba mumewe akitika asubuhi kwenda kazini hana amani. Anatamani aende naye. Anashinda nyonge na hata chakula hakitamani. Anawaambia walimwengu wamwache afanye wivu kwa mpenzi wake. Bila wivu atajuaje kama kweli anampenda?

Mume anamwambia mkewe apunguze wivu ili kazi iendelee, kwani penzi la kushinda ndani hawatoliweza.

**Wivu-DDC Mlimani Park**

Ilikuwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, DDC Mlimani Park ilirekodi wimbo uitwao 'Wivu'. Huyu sasa ni mwanamume. Mke anamshangaa mumewe kuwa amebadilika. Amekuwa na wivu kupindukia, kwani hata akiwa kazini haishia kuaga na kuja kumchunguza nyumbani. Anadai hata akienda sokoni humfuata nyuma kuchunguza amesimama na nani.

Mume anamjibu siyo wivu, ila anaona uchungu kusikia maneno kwa majirani, kwa hiyo ana wasiwasi.

**Wivu-Kurugenzi Jazz Band**

Huu ni wimbo wa mwishoni mwa miaka ya 1970. Ulipigwa na Kurugenzi Jazz Band. Jamaa anawaasa wanaume waache wake zao waende kazini wakafanye kazi. Baadhi ya waume wamekuwa wakiwakataza wake zao kufanya kazi. Tatizo si lingine ni wivu tu.

Mtunzi anasema maisha ya leo ni mke na mume kusaidiana na si kuwaweka akinamama nyumbani tu.

**Stendi ya Basi-Tomatoma**

Kwenye wimbo huu wa miaka ya 1980, ni kwamba jamaa anamuuliza mkewe ambaye ni mfanyakazi kwa nini siku hizi amekuwa akirudi usiku?

Mke anamjibu anachelewa stendi ya basi kwa sababu kuna tabu sana ya usafiri. Nadhani ingekuwa miaka ya sasa mke angesema foleni. Haya yote ni mambo ya wivu.

**Ilikuwa Lifti Tu-Vijana Jazz Band**

Bendi ya Vijana Jazz katikati ya miaka ya 1980, ilitoka na kibao kiitwacho 'Ilikuwa Lifti Tu'. Ulikuwa ni utunzi wa Hamza Kalala.

Mke anajitetea kwa mumewe kuwa kijana aliyekuwa naye ndani ya gari alimsaidia kusukuma gari lake, hivyo alimpa lifti na hakuna kingine kilichokuwa kinaendelea.

Mume anajibu tatizo siyo lifti, ila ni tabasamu na vicheko vilivyokuwa ndani ya gari, ndivyo vilivyomchanganya na kuona anaibiwa.





# Lilian, Ubi wapeana talaka rasmi

HATIMAYE ndoa ya mwigizaji maarufu kutoka Nollywood, Lilian Esoro, na mume wake Ubi Franklin, imefikia ukingoni.

Kulingana na mtandao wa Pulse, nyaraka inayoonyesha wanandoa hao wamepeana talaka imevuja na kuchapishwa katika blogu moja ya Linda Ikeji, ikieleza ndoa hiyo ilifikia tamati Januari 28, mwaka huu katika Mahakama Kuu ya Abuja.

Mwaka 2019, mahakama hiyo iliamuru wawili hao kuendelea kuishi kama mume na mke baada ya Lilian, kueleza Ubi amebadili mwenendo na anatunza vyema familia ake.



## T.I ashambuliwa Twitter

RAPA maarufu wa Marekani, T.I. amejikuta akiwasha moto kwa wafuatiliaji wa mtandao wa Twitter, baada ya kutokea na mwonekano mbaya katika filamu aliyoigiza ya 'Cut Throat City'.

Katika filamu hiyo, T.I. amecheza akionekana ana ugonjwa wa ngozi unaosababisha kuwa na mabaka meupe usoni unaojulikana kama Vitiligo.


Baadhi ya watu walimsakama kwa kucheza akiwa na tatizo hilo huku wengine wakisema hakucheza vizuri katika filamu hiyo na kuonekana kama anajifunza.


## Selento mbaroni kumuua mjomba wake

MWANAMUZIKI wa hiphop kutoka Marekani, Ricky Hawk, maarufu kama Silento, amefunguliwa mashtaka ya kuua mjomba wake.

Rapa huyo kwa sasa anashikiliwa katika gereza la DeKalb County, baada ya kudaiwa kumuua Fredirick Rooks, ambaye ni ndugu yake.

Taarifa ya kukamatwa kwake ilitolewa kupitia ukurasa wa Twitter wa polisi wa jimbo la DeKalb siku ya Jumatatu.





## Meghan abadili jina la mtoto wake

MKE wa mwana mfalme wa Uingereza, Meghan Markle, ameamua kutuliza hali ya hewa baada ya kusema hatua ya kubadilisha jina la mtoto wao katika cheti cha kuzaliwa imepitishwa na himaya ya kifalme.

Meghan ambaye ni mwigizaji wa filamu na mwana Mfalme Harry, walifunga ndoa ya kihistoria mwaka 2018.

Kulingana na mtandao wa PageSix, msemaji wa mwanamfalme huyo, alisema kubadilishwa kwa jina hilo kuwa "Rachel Meghan," kutoka Archie, ilipewa Baraka na mamlaka ya kifalme.

Kabla ya kubadilisha jina hilo, cheti chake cha kuzaliwa kiandikwa jina la Archie Harrison Mountbatten-Windsor.

## Zlatan eti hajui aliyemfungia mpenzi wake

RAPA mkali wa Nigeria, Zlatan Ibile, kwa mara ya kwanza amemzungumzia mpenzi wake DJ Cuppy, akisema hajui ni nani alimfungia wasiwasiliane kupitia mitandao ya kijamii.

Awali, DJ Cuppy, alieleza kwamba ana wasiwasi rapa huyo aliamua kumfungia wasiwasiliane kupitia uwanja huo wa mitandano.

Akihojiwa katika kipindi cha 'TheSwitch', mwanamuziki huyo amesema "Ukiniuliza suala hilo najibu sijui nani alimfungia Cuppy,"



# HUYU NDIYE DOMINIC ONGWEN

- Aliogopwa Uganda kwa ukatili wake
- ICC yamuhukumu kuua, kubaka, utumwa



Dominic Ongwen.. **PICHA: MTANDAO**

MAELFU ya watu waliopitia ukatili wa kutisha kutoka kundi la Lord's Resistance Army (LRA), wamepewa haki baada ya kiongozi wa waasi hao kukutwa na hatia.

Kiongozi hiyo wa waasi, Dominic Ongwen, amesomewa hukumu ya awali na Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) na kupatikana na hatia ya utesaji, mauaji na ubakaji.

Ongwen, ambaye alikuwa kamanda anayeogopwa sana na wananchi wa Uganda, ni mfuasi wa kwanza kutoka kundi hilo kufikishwa katika mahakama hiyo ya kihalifu.

Kamanda huyo namba mbili, alikabiliwa na makosa 70 ya uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita, lakini baadhi yaliondolewa kutokana na kukosa ushahidi.

Mashtaka yote yalihusu kuhusika na shambulio kwenye kambi ya wakimbizi wa ndani nchini Uganda mnamo 2004.

Hata hivyo, kuna wakati kesi hiyo ilingia katika utata baada ya kuonekana mtuhumiwa huyo kuwa ni mwathiriwa wa utekaji nyara na pia mhalifu.

Wakati wa utetezi wake, Ongwen, alisema akiwa mtoto alitekwa na LRA na kulazimishwa kuwa mwanajeshi, kabla ya kupanda nafasi na kushika Naibu kamanda nyuma ya Joseph Kony ambaye alikuwa kamanda mkuu.

Akisoma uamuzi wake, jaji anayesimamia kesi hiyo Bertram Schmitt alisema licha ya utetezi wake Ongwen ana hatia ambayo imethibitishwa bila shaka yoyote.

Baadhi ya makosa ambayo alikutwa na hatia ni uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya ubinadamu, mateso, utumwa wa kingono na uporaji.

ICC ilitoa hati ya kukamatwa kwake mwaka 2005, vikosi vya majeshi ya Marekani na rika wamekuwa wakimtafuta tangu mwaka 2011.

Mwaka 2014 alijisalimisha nchini Jamuhuri ya Afrika ya Kati na kesi yake imedumu kwa miaka mitatu na nusu katika makao makuu ya mahakama hiyo mjini The Hague, Uholanzi.

Mawakili wake walijitahidi kuweka hoja ya kuachiliwa kutokana na makosa yote aliyafanya kutokana na shinikizo.

Wakiongea na shirika la habari la Reuters, walisema Ongwen alitekwa nyara na katika matukio hayo hakuwa na cha kufanya, alifanywa mtumwa.

"Utumwa huo uliendelea hadi alipoondoka msituni." Amesema mmoja wa mawakili wake.

Lakini waendesha mashtaka walisisitiza kuwa alikuwa mtu mzima wakati akifanya makosa hayo, hivyo haiwezekani kutowajibishwa.

**DOMINIC OGWEN NI NANI?**

Dominic Ongwen alizaliwa mwaka 1975 katika kijiji cha Choorum, Wilaya ya Amuru Kaskazini mwa Uganda.

Kwa mujibu wake, akiwa na miaka 14 alitekwanyara na kundi la waasi wa Josephy Kony wakati akielekea Shule ya Msingi Abili Koro mwaka 1988.

Hata hivyo, ripoti sahihi zinasemekana wakati anatekwa alikuwa na umri kati ya miaka 9 na 10.

Kutokana na ripoti hiyo, Ongwen alibebwa katika safari yao hadi kwenye kambi ya LRA, alikuwa hawezi kutembea.

Mama yake Ongwen alipofahamishwa habari za kutekwanywara kwa mtoto wake, aliamua kuwafuata wafuasi hao, lakini alikutwa mama huyo amefariki dunia akiwa pamoja na mumewe.

Baada ya kukua mikononi mwa waasi, akiwa na umri wa miaka 18, Ongwen alipewa cheo cha Brigedia wa kundi la LRA na kuongoza kikosi cha Sinia.

Ogwen alishiriki katika matukio mbalimbali ya uhalifu wa kivita mwezi wa Mei, mwaka 2004, waliposhambulia kambi ya ndani ya Lukodi iliyoko Wilaya ya Gulu Kaskazini.

Pia alishambulia kambi nyingine za ndani ikiwamo ya Pajule, Odeke na Abok na kushiriki mauaji mbalimbali ya wananchi wasiokuwa na hatia, ubakaji na unyanyasaji wa kingono.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**



Kamanda Ongwen akiwa katika harakati za kundi lake msituni.

MAKALA

# MARA INAVYOPANIA KUJIIMARISHA KIUCHUMI KUPITIA KAHAWA, IMEANZA NA WILAYA NNE

**Na Sabato Kasika**

HIVI karibuni, Mkoa wa Mara ulizindua mkakati wa uhamasishaji na usimamizi wa kilimo cha zao la kahawa kwa lengo la kuinua uchumi wa wakulima, mkoa na taifa kwa ujumla.

Mkakati huo ambao umejikita zaidi katika kushirikiana na wadau mbalimbali, kwa ajili kufanya mapinduzi ya kilimo ndani ya mkoa huo, ulizinduliwa na mkuu wa mkoa huo Adaam Malima.

Baadhi ya wadau hao wa sekta ya kilimo Malima anawataja kuwa ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo Nchini (TADB), Bodi ya Kahawa na Taasisi ya Utafiti wa zao la Kahawa (TaCRI), ambapo TADB itatoa fedha.

Akizundua mkakati huo, Malima anasema, mkoa umeshatangaza kahawa kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati yatakayotumika kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja, mkoa na taifa kwa ujumla.

Kwamba, wanataka wazalishe wa miche ya kahawa zaidi ya milioni, ambayo itakuwa na uwezo wa kuzalisha kilo tatu hadi nne za kahawa kwa mche na pia wakulima kupewa elimu kuhusu kilimo cha kisasa.

"Ushauri wa kitaalam utatolewa na TaCRI, huku msimamizi akiwa ni Bodi ya Kahawa, na ili mkakati huu ufanikiwe, yapo mambo mbalimbali ambayo mkoa umepanga kuyafanya," anasema Malima.

Anasema, kwa muda mrefu mkoa huo umekuwa ukilima kwa kiasi kidogo cha kahawa aina ya Arabika, hasa katika Wilaya za Tarime, Rorya na Butiama, lakini imekuwa na ubora mkubwa na kufanikiwa kuongoza kwa ubora Afrika.

Kwa mujibu wa Malima, sasa mkoa umeamua kuingia rasmi katika uzalishaji wa zao hilo na kwamba, kama wakulima watapata usimamizi mzuri wa mashamba yao, kahawa itawakomboa kiuchumi.

**MATARAJIO**

Mkuu huyo wa mkoa anasema, matarajio yao ni kwamba, iwapo mkakati huo utafanikiwa, mkulima ataweza kupata zaidi ya Sh. milioni tano kwa ekari moja ya kahawa, na kuwataka wadau wote waendelee kuunga mkono mkakati huo.

Pia anasema, lengo la mkoa ni kutekeleza kwa vitendo mkakati huo kwa kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 2,000 hadi kufikia tani 15,000 ndani ya miaka minne ijayo.

Anasema, mwaka jana, alipokea miche ya kahawa 40,000 iliyotolewa na Bodi ya Kahawa nchini (TCB) ikiwa ni sehemu ya miche 100,000 ambayo bodi hiyo iliahidi kutoa kwa ajili ya kupandwa katika mashamba mbalimbali.

Anafafanua, zao la kahawa kwa sasa linalimwa katika wilaya za Tarime, Butiama, Serengeti na Rorya, kwa vile ndio maeneo ambayo limeonyesha kustawi kwa wingi.

"Tunataka tuwe mfano katika kilimo bora cha kahawa hapa nchini, tumeanza na tunazidi kuendelea. Lengo letu ni kupanda miche angalau milioni mbili kila mwaka katika mkoa mzima," anasema.

HALI YA MKOA

Anasema, mkoa wa Mara una eneo la kilomita za mraba 30,150. Kati ya eneo hilo, kilomita za mraba 10,942 ni eneo la maji, sawa na asilimia 36 na kilomita za mraba 19,208 sawa na asilimia 64 ni eneo la nchi kavu.

"Katika eneo la nchi kavu, kilomita za mraba 9,452.34 sawa na asilimia 49.2, ziko katika hifadhi za wanyamapori, ikiwamo Hifadhi ya Taifa Serengeti na Mapori ya Akiba ya Ikorongo," anaasema.

Anataja maeneo mwengine yaliyomo kuwa ni Hifadhi za Jamii Grumeti na kwamba eneo linalobaki ni kilometa za mraba 9,755.66 sawa na asilimia 50.7 ya eneo la nchi kavu kwa ajili ya kilimo, mifugo na makazi.

Malima anataja baadhi ya mazao makuu ya chakula na biashara ambayo hulimwa kwa wingi mkoani mwake kuwa ni mahindi, mtama, viazi vitamu, maharage, mpunga, ndizi na mhogo.

"Sasa tumeona kuna haja ya kuimarisha zao la kawaha ambalo halikuwa na umaarufu mkoani kwetu, tumelifanya la kimkakati kwa ajili ya kuinua uchumi wa wakulima, mkoa na taifa kwa ujumla," anasema.

Aidha, anasema, uchumi wa mkoa huo unategemea zaidi kilimo, ambacho huchangia kiasi cha asilimia 60 ya pato la mkoa, huku sekta nyingine, ambazo huchangia katika uchumi huo zikiwa ni mfugo, madini uvuvi na utalii.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, akiwa na moja ya miche ya kahawa

**BODI YA KAHAWA**

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa, Prof. Jamal Katundu anasema, Tanzania ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 50,000 za sasa hadi tani 200,000 ndani ya kipindi cha miaka mitano ijayo.

Katika kufanikisha hilo, anasema bodi hiyo ina mpango wa kushirikiana na halmashauri za wilaya kupanda mashamba mawili makubwa ya mfano katika kila wilaya inayolima kahawa.

"Mashamba hayo yatatumika kama mashamba darasa kwa wananchi wanaoyazunguka, lakini pia ninaushukuru Mkoa wa Mara kwa utayari katika kuongeza uzalishaji wa kahawa," Prof. Katundu anasema.

Prof. Katundu anasema, uongozi wa serikali mkoani humo umekuwa ukihamasisha kilimo cha kahawa, ambapo anaitaka mikoa mingine inayolima zao hilo kuiga mfano huo.

"Mkoa wa Mara umekuwa kinara katika uhamasishaji na usimamizi wa kilimo cha zao hilo, mikoa mingine inapaswa kuiga na kujifunza yale yanayofanywa na uongozi wa Mkoa wa Mara," anasema.

Aidha, anasema, bodi yake imejiwekea malengo muhimu ya kuongeza uzalishaji wa kahawa nchini, kuhakikisha kunakuwa na bei nzuri, na kujenga mazingira bora ya biashara kwenye tasnia ya kahawa.

"Bodi ya Kahawa itaendelea kusimamia na kutekeleza maagizo ya serikali ikiwamo upatikanaji wa miche bora kwa wakulima, malighafi kwenye viwanda vya kahawa na kuhakikisha mkulima anapata bei nzuri kupitia kuongeza ushindani kwenye soko la kahawa la awali na soko la pili.

**KAHAWA NCHINI**

Hapa nchini, kahawa hulimwa sehemu tofauti zikiwamo za miteremko kama ya Mlima Kilimanjaro, kusini mwa Mlima Meru, Nyanda za juu za Ngorongoro na miteremko ya milima ya Uluguru.

Vilevile hulimwa katika Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kasulu, Kibondo), Mkoa wa Mbeya wilaya za Rungwe, Mbeya, Mbozi na Tanga katika miteremko ya milima ya Usambara.

Inaelezwa kuwa zao hilo huwa tayari kuvunwa miezi nane hadi tisa tangu kipindi ambacho maua yamechomoza, hutakiwa kuvunwa matunda yale ambayo yakishaiva hubadilika rangi kua nyekundu.

Kwa mujibu wa Meneja wa Taasisi ya Utafiti wa zao la Kahawa (TaCRI), Kanda ya Ziwa Sirari, Almas Ahmad, kahawa hustawi vizuri kwenye udongo wenye asili ya volcano ambao haujawahi kulimwa.



Baadhi ya viongozi wa mkoa huo wakiangalia mkahawa walipotembelea moja shamba la zao hilo wilayani Tarime. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Biden aahidi mapya barani Afrika

**Washington,** MAREKANI

RAIS Joe Biden amesema yuko tayari kujenga upya uhusiano na Umoja wa Afrika (AU).

Rais Biden aliahidi kujenga upya ushirika wa nchi hiyo na AU, muda mchache baada ya kutoa hotuba ya kwanza kuhusu sera za mambo ya nje tangu kuingia madarakani.

Mtangulizi wake, Donald Trump, alizusha mgogoro mwaka 2018 kwa madai ya kutumia maneno ya fedheha alipoyaelezea mataifa ya Afrika.

Trump baadaye alikana madai kuwa yeye ni mbaguzi wa rangi.

Siku ya juzi, Ikulu ya White House ilitweet video ya matamshi ya Rais Biden kuhusu bara la Afrika, kabla ya mkutano wake wa 34.

"Utawala wangu unajitoa kujenga tena ushirika wetu duniani na kujihusisha tena na taasisi za kimataifa kama vile Umoja wa Afrika."

"Pia lazima tukabiliane na changamoto kubwa zilizopo. Hiyo ni pamoja na kuwekeza zaidi katika afya ya ulimwenguni, kuishinda Covid-19 na kufanya kazi ya kuzuia, kugundua na kushughulikia shida za kiafya za siku zijazo.

Kushirikiana na kituo cha kupambana na magonjwa cha Afrika CDC na taasisi zingine kuendeleza usalama wa afya," alisema Rais Biden. **BBC**



Rais wa Marekani, Joe Biden. **PICHA: BBC**

## Maandamano kupinga mapinduzi yaongezeka Myanmar

**Naypyidaw,** MYANMAR

MAANDAMANO yameongezeka nchini Myanmar dhidi ya mapinduzi yaliyofanyika Jumatatu wiki hii, licha ya juhudi za jeshi kuonyesha kuwa linachukua udhibiti wa taasisi za nchi hiyo.

Wabunge wapatao 70 kutoka Chama cha National League for Democracy (NLD), kinachoongozwa na Aung San Suu Kyi walifanya mkutano katika mji mkuu wa nchi hiyo Naypyidaw kuonyesha pingamizi zao kwa mapinduzi hayo.

Kundi moja la raia linasema waandamanaji walikabiliana na wanajeshi katika mji mkubwa wa Mandalay, Alhamisi na kusababisha majeruhi.

Wakati huo huo, runinga inayoendeshwa na serikali ya nchi hiyo, iliripoti kwamba Mkuu wa Majeshi, Jenerali Mwandamizi Min Aung Hlaing, alikutana na maofisa wa benki na wengineo kutafuta ushirikiano wao ili kuimarisha uchumi wa nchi hiyo na maisha ya watu.

Khin Zaw Win, mshauri mchambuzi wa nchi hiyo aliyeishauri serikali ya Myanmar, aliiambia NHK kwamba jeshi lilifanya mazungumzo na upande wa Aung San Suu Kyi siku mbili kabla ya mapinduzi hayo.

Alisema upande wa Aung San Suu Kyi ulikataa kufanya uchunguzi wa udanganyifu ambao jeshi linadai ulifanywa wakati wa uchaguzi mkuu mwaka jana.

Mamia ya walimu na wanafunzi jana, walifanya maandamano katika chuo kikuu cha Myanmar dhidi ya mapinduzi ya kijeshi yaliyosababisha kuondolewa kwa kiongozi wa nchi hiyo Aung San Suu Kyi.

## Biden afuta msaada wa kijeshi Yemen

**Washington,** MAREKANI

RAIS Joe Biden ametangaza mwelekeo mpya wa siasa za nje za Marekani, akidhamiria yaliyoachwa na watangulizi wake.

Biden ameondoa msaada wa Marekani kwa muungano wa kijeshi nchini Yemen.

Alitangaza hatua hiyo ya serikali yake, kwamba msaada kwa mashambulizi ya kijeshi yanayoongozwa na Saudia Arabia nchini Yemen ambayo yameongeza mateso katika taifa hilo.

Rais Biden aliitaja hatua hiyo kama sehemu ya Marekani ya kudumisha msisitizo wa nchi hiyo kuhusu diplomasia, demokrasia na haki za binadamu.

Wakati wa ziara yake ya kwanza katika Wizara ya Mambo ya Nje kama rais, Biden aliwaambia wanadiplomasia kuwa vita hivyo vimesababisha janga la kibinadamu na la kimkakati na kwamba lazima vimalizike.

Maamuzi hayo kuhusu Yemen ni moja kati ya mikakati iliyotolewa na Biden hapo juzi ambayo alisema inalenga kubadilisha mwelekeo wa sera ya mambo ya nje ya Marekani.

# Jela miaka 15 unyanyasaji kingono dhidi ya wasichana

**Pennsylvania,** MAREKANI

MMISHIONARI wa Marekani amehukumiwa kifungo cha zaidi ya miaka 15 gerezani kwa makosa ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya wasichana wadogo.

Hilo lilitokea kituo cha watoto yatima cha Bomet nchini Kenya alichokuwa akiendesha pamoja na mke wake.

Gregory Dow (61), alikubali kutekeleza makosa hayo ya uhalifu wakati kesi hiyo iliposikilizwa katika Jimbo la Pennsylvania.

Mashtaka dhidi ya Dow yalieleza kuwa alipoanza kunyanyasa wasichana wadogo, wawili kati yao walikuwa na umri wa miaka 11 na 12, huku mwingine akiwa na umri wa miaka 13.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa, Dow, alijifanya kuwa mkristo mmishionari ambaye angetunza watoto hao waliokuwa yatima, ambao walimwita baba.

Alidai, badala ya kuwa baba kwao, aliwanyanyasa ujana wao na kutumia hali yao ya uhitaji vibaya.

"Alitumia nguvu na kushurutisha watoto kutekeleza vitendo hivyo vya kikatili na uhalifu, aliyemelea wasichana wadogo waliokuwa na uhitaji kwa kujifurahisha kingono," waendesha mashtaka walisema.

Kituo cha watoto yatima cha Dow huko Boito, kilianzishwa mwaka 2008, na kufungwa mwaka 2017.

Mwaka 2008, Dow alianzisha makao ya watoto yatima Magharibi mwa Kenya.

Makao hayo pia yalikuwa yanasimamiwa kwa pamoja na makanisa kaunti ya Lancaster Jimbo la Pennsylvania, nchini Marekani kulingana na gazeti la eneo la LNP.

Shirika la Upelelezi Marekani (FBI) na mamlaka ya Kenya zilimchunguza mtuhumiwa na akafikishwa mahakamani nchini Marekani.

Mmishionari huyo alitoroka Kenya, Septemba mwaka 2017 baada ya kuibuka kwa madai ya unyanyasaji.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MASHAMBA/DODOMA

**MASHAMBA YANAUZWA DODOMA TANZANIA** : Wasiliana sasa na Dodoma Pazuri Group (DPG). Karibu Dodoma, Karibu Makao Makuu. Tupigie Simu No: **0759 848 155 / 0745 312 893**

## VIWANJA/KIBAHA

**VIWANJA VINAUZWA KIBAHA:** Ukubwa wa Viwanja ni Urefu Mita 20 kwa Upana Mita 20. Wasiliana na Kibaha Pazuri Group (KPG). Tupigie Simu: **0654 291766 / 0657 990015**

## NYUMBA/MBEZI

**NYUMBA ZINAUZWA MBEZI :** Je? unataka kununua nyumba Mbezi. Utanunua nyumba kwa haraka Wasiliana na Mbezi Pazuri Group (MBEPA). Tupigie: **0654 291766 / 0657 990015**

## NYUMBA/KIBAHA

**NYUMBA ZINAUZWA KIBAHA - PWANI:** Kibaha Maili Moja, / Kibaha Kwa Mathias / Kibaha Kwa Mfipa / Kibaha Misugusugu. Tupigie Simu: **0654 291766 / 0657 990015**

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## TANGAZO LA MNADA/NOTISI

**TULVIN INVESTMENT. CO. LTD** kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD** tunatoa notisi ya madai ya siku kumi na nne (14) kwa ndg **Abdul Hashim Said** ambaye ni mdaiwa sugu kuwa uwe umelipa deni lako unalodaiwa na **Tujijenge Tanzania Ltd** pamoja na gharama zote za dalali tangu siku ya tangazo hili.

Kushindwa kulipa tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara nyumba uliyoweka dhamana ya mkopo iliyopo Mbondole kwa Mhaya kwa mujibu wa sheria. Mnada utafanyika kuanzia saa nne (4 mara baada ya gari la matangazo sehemu mali husika ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalipa 25% siku ya mnada na 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa salio halirudishwi na mnada utarudiwa.
2. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**MAWASILIANO PIGA: 0625589850/0753191755/0686908882 au Email: tulvininvestment@gmail.com**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

Ndugu **ATHONY MICHAEL MYOMBO** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya bajaji Yenye usajili namba **MC 415 BWZ** aina yake **TVS .**
Kwa yoyote atakae ona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi.
RB no;
**MOR/MOR/RB/70118/2021**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi NA.12/2021**

**Ombi la (1) DORIS JOHN ANDONDILE na (2) DONARD BENEDICT kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu BENEDICT DONALD**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/2/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 28/1/2021

Tarehe 28/1/2021
Sahihi ya Hakimu

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.Na.MMC/LD/5061. Tarehe: 05/02/2021**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MMC/LD/5061**
**MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: ASHA MASHAKA MAYUWE**
**ARDHI: KIWANJA NA. 428 KITALU 'B' KOLA HILL B**
**MUOMBAJI: ASHA MASHAKA MAYUWE**

Taarifa inatolea kwamba BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na inakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI iwapo hakuna pingamizi Litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapo tangazwa katika Gazeti.
HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO ikionekana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO

Mamuya, G.C
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICTOR AMBROSE MAGANYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T514 AFA** chasisi namba **FE437EV442296,** engine namba **4D33882647,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa CONTROL NUMBER **9910820417229**


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yoyote zaidi yao. Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani?

Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

## Lazima Apatikane-7




**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Gari iliingia kwenye nyumba moja ambayo ilionekana ni kama ofisi na si nyumbani kwa Martin kama alivyosema hapo mwanzo.

"Karibu, ingia ndani." Alimkaribisha.

"Shukrani", Mwanaidi alijibu.

Akajipweteka kwenye kiti kimoja kikubwa, kinene, kirefu, wakati Mwanaidi akiwa bado amesimama.

"Kaa hapo." Alimwonyesha kwenye kiti kimoja ambacho kilikuwa kinatazamana na yeye.

Mwanaidi akakaa na kutazamana uso kwa uso na Martin. Tayari uso wake ulianza kuingia mashaka.

"Nimekuchukua nyumbani kwako na kukuleta hapa kwa sababu kuna kazi moja nataka nikupe." Martin alisema huku akijitingisha kwenye kiti hicho cha kuzunguka.

"Kazi gani." Mwanaidi aliuliza kwa mshangao kwa sababu awali alivyoambiwa ni tofauti na sasa.

"Kazi ndogo tu ya mara moja."

Mwanaidi alihisi ganzi kwenye mwili wake, kwani alihisi huenda kuna kitu ambacho si cha kawaida.

Kuambiwa anakwenda kupewa vitu vya marehemu mpenzi wake na pesa zake, halafu sasa anaambiwa anataka kupewa kazi, vilimfanya kuchanganyikiwa na akanyamaza, akisubiri ni kazi gani atapewa.

"Ni kazi ya kuua mtu."

"Kuua mtu?" Mwanaidi alijikuta akiropoka kwa nguvu na kwa mshangao.

"Kwani ni kazi kubwa sana kwako? Mbona ni rahisi sana? Kwani wewe hujawahi kuua mtu?" Yalikuwa ni maswali ya Martin yalioonekana kama ya mzaha, lakini yalimtisha mno Mwanaidi kiasi cha kijasho chembamba kuanza kumtoka.

"Miezi miwili tu iliyopita umetoka kumuua mpenzi wako Burhan kwa kisu, tena kwa mkono wako, na sasa una kesi ya mauaji. Sijui umehonga nini hadi uko nje kwa dhamana, itakuwa kumuua mtu ambaye humjui?"

"Sijaua mimi."

"Umeua dada dunia nzima inajua na nataka uue tena, safari hii hakuna atakayejua kama wewe umeua."

"Siui mimi."

"Utaua kwa lazima, vinginevyo sasa utakufa wewe. Kumbuka uko kwenye mikono yangu kwa sasa."

Mwanaidi alibaki kimya. Aliona sasa dunia yote imemwelemea.

Hakuona raha ya kuishi, kwani kila kukicha yeye ni matatizo.

Baada ya kutolewa, alidhani angepumzika, lakini kinachotokea hapo ni kielelezo kingine kuwa yeye amezaliwa akiwa na bahati mbaya tu.

Alijuta hata kukubali kutoka rumande ambako alichokosa ni uhuru tu. Lakini kila kitu alikuwa nakipata.

"Sikiliza we mwanamke. Usitake nilazimike nikupige. Mimi huwa sipigi wanawake wazuri kama wewe. Nachotaka umuue mtu mmoja ambaye usiku huu atakuwa yupo baa anakunywa. Ukishamaliza kumuua nakuachia huru, tena nitakupa na zawadi na pesa kiasi kadhaa ambazo hujawahi kuzipata kwenye maisha yako." Martin alimuahidi Mwanaidi.

"Sawa naweza kuua, lakini..."

"Hakuna lakini Mwanaidi. Ni kwamba ukimuua mimi nitahakikisha unakuwa salama. Hakuna yoyote atakayekukamata, ila kukikataa, kichwa chako ni halali yangu." Alitishia.

"Kumbuka kuwa umeshaua mtu. Umemuua rafiki yangu Burhan ambaye nilikuwa namtegemea kwenye mambo yangu mengi."

Mwanaidi alitetemeka mwili mzima. Lakini hakuwa na jinsi. Ni kukubali ili awe hai. Hakutaka kupoteza uhai akiwa bado msichana mbichi.

"Nifanyeje sasa?" Aliuliza Mwanaidi.

"Hujui ufanyeje? Umuue na huyu kwa kisu kama ulivyomuua Burhan."

Ni maneno yaliyokuwa yakizidi kumtisha Mwanaidi.

"Hapana mrembo." Martin alimshusha presha Mwanaidi. "Hutomuua kwa kisu. Itakuwa kazi ndogo tu, tofauti na ile ya Burhan. Huyu nataka awe kwa kumwekea sumu kwenye kinywaji." Alisema Martin kama kwamba anapanga mipango ya kwenda kukata tiketi ya ndege ili asafiri.

"Nitakutana naye vipi?" Mwanaidi aliuliza na kusababisha kicheko kutoka kwa Martin. Kwa mara ya kwanza Mwanaidi kumuona Martin akifurahi. Ilimshangaza na kumtisha kwa wakati mmoja.

"Nimekwambia kazi yako ni ndogo sana. Kuua. Asilimia tisini tayari nimeshafanya mimi. Ni kwamba leo jioni marehemu mtarajiwa atakuwa anakunywa kwenye baa moja hivi mitaa ya Tandika. Huyo anapenda sana vimwana. Nimemuahidi kumletea mrembo wa shoka. Ni rafiki yangu na nitakwenda na wewe hadi pale. Nachotaka ni kwamba baada ya kunywa, mtaelekea kwenye vyumba vya kulala vilivyomo kwenye baa hiyo. Humo muende na vinywaji vyenu, utamuwekea dawa kwenye pombe na wewe kazi yako itakuwa imeisha."

"Ni dawa ya aina gani kaka?"

"Ni hii hapa." Martin alifungua droo na kutoa pakti moja nyeupe.

"Hii ni dawa kwa upande mwingine ni sumu. Hata ukiishika haina madhara, ila ikishaingia kwenye pombe inageuka kuwa sumu."

**"Hii ni dawa kwa upande mwingine ni sumu. Hata ukiishika haina madhara, ila ikishaingia kwenye pombe inageuka kuwa sumu."**

"Hawezi kunishtukia?"

"Atakuwa ameshalewa. Na wewe kwa sababu nia yako ni kumtilia sumu, sidhani kama utakunywa kwa kufakamia. Pia mimi nitakuwapo hapo, ingawa nikikukabidhi kwake nitadanganya kuwa naondoka kuna kazi nakwenda kufanya."

Ilikuwa bado kidogo, Mwanaidi aulize sababu ya kumuua mtu huyo, lakini akasita kwani, kazi aliyopewa ni kuua tu na si kuuliza sababu ya kuuawa kwa mtu huyo.

"Kitu cha kwanza kabisa ambacho kitafanyika tukitoka hapa ni kukupeleka saluni. Utakwenda kujipamba huko kwenye saluni za bei kubwa, siyo kama zile zenu au ile unayofanyia kazi kule Mburahati. Yaani nataka uonekane kama malaika. Tika akikuona achanganyikiwe. Tena na wewe ulivyokuwa mzuri, na watakavyokupamba, mbona atakufa vizuri tu."

"Mimi nimekubali, cha muhimu unihakikishie usalama tu." Mwanaidi aliongea kwa sauti ya chini akionekana kukubali, ingawa ilionekana kwa mbali kuwa ni shingo upande.

"Hilo halina neno, ila nakusisitizia tena. Sitaki lawama we mwanamke. Kwanza ukifika pale uchangamke. Usionyeshe kama kuna kitu unacho moyoni, au umelazimishwa kwenda pale. Kitendo chochote cha kushindwa kutekeleza jambo hili ni kwamba utakuwa tayari umeshajikatia tiketi ya kwenda ahera kuungana na mpenzi wako Burhan ili kwenda kujibu tuhuma za kwa nini ulimuua."

***Itaendelea Jumamosi***



# ALLEGRI

## ATAJWA KUMRITHI ZIDANE

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wanaripotiwa kuwa wanamtazama kocha wa zamani wa AC Milan na Juventus, Massimiliano Allegri kama mrithi wa Zinedine Zidane katika kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

Mustakabali wa Zidane, raia wa Ufaransa kwa Los Blancos hao unaonekana kutokuwa na uhakika, kwa sababu ripoti nchini Hispania zinadai atabadilishwa mwishoni mwa msimu huu.

Redio Cadena SER imeripoti kuwa mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo, Raul Gonzalez, ambaye kwa sasa ni kocha wa timu ya vijana ya Real Madrid, pia anaangaliwa kuwa mrithi wake.

Tofauti ya Allegri na Raul ni uzoefu wa muda mrefu kwenye nafasi hiyo ya ukocha.

Wakati Allegri amezifundisha klabu kadhaa kubwa, Raul bado hajafikia kwenye kiwango hicho.



## KOEMAN AMJIA JUU DI MARIA

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronard Koeman, amemtaja Di Maria kama hana heshima, hii ni baada ya kusema ana imani Lionel Messi ataungana naye katika kikosi cha PSG.

Messi anamaliza mkataba wake ndani ya Barcelona mwisho mwa msimu huu na kumekuwa na hali ya sintofahamu kuhusu hatima yake baada ya mkataba huo kumalizika.

PSG watapambana na Barcelona kwenye hatua ya 16 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi itakayofanyika Februari 16, mwaka huu.

"Ndio, ndio, ninaamini hivyo. Kuna uwezekano mkubwa. Tunapaswa kuwa watulivu wakati huu ambapo mambo mengi yanaendelea," alisema Di Maria baada ya kuulizwa kama Messi ataungana nae pale Paris.

"Sio sawa kuongea kitu kama hicho, hasa wakati huu ambao tunakutana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ninadhani sio sawa na ni kukoseana heshima, kumwongelea mchezaji mmoja ambaye bado ni mchezaji wa Barcelona," alisema Koeman kuhusu alichokisema Di Maria.

## LIVERPOOL YAZIDI KUPATA MAJANGA

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kwamba, Diogo Jota bado atakuwa nje kwa wiki kadhaa, lakini Sadio Mane anaweza kuwakabili Manchester City.

Nafasi ya wekundu hao kutetea ubingwa wa Ligi Kuu England msimu inaelekea kuwa ngumu baada ya kupokea vipigo mfululizo katika mechi zake mbili zilizopita.

Jota amekuwa nje ya dimba tangu Desemba, mwaka jana kutokana na jeraha la goti, wakati Mane alikosa michezo miwili ya Liverpool iliyopita kutokana na jeraha la misuli.

Baada ya mchezo na Brighton kumalizika Klopp alikuwa na habari juu ya wawili hao.

"Diogo Jota sijui ni lini haswa atakuwa sawa, wiki kadhaa, mbili, tatu, nne. Sina hakika," aliwaambia waandishi wa habari.

"Na Sadio Mane tutaona, anaweza kupatikana kwa wikendi hii, sijui hajafanya mazoezi na timu bado, Tutaona."





# MOURINHO BADO ANA IMANI NA SPURS

**LONDON, England**

LICHA ya kikosi cha Tottenham kupoteza mchezo wake wa Ligi Kuu England kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Chelsea, juzi Alhamisi, Jose Mourinho, kocha mkuu wa timu hiyo amesema anaona 'moyo wa upambanaji' kwa wachezaji wake.

Tangu iliposafiri kuibukia ndani ya Anfield, Desemba 16, mwaka jana, Tottenham imepoteza jumla ya mechi tano kati ya tisa, ambazo imecheza na mitatu kati ya hiyo imekuwa ni mfululizo tangu kuanza kwa mwaka huu.

Matokeo hayo kwenye mechi za Ligi Kuu England ilikuwa kichapo cha mabao 3-1 na Liverpool, Brighton 1-0 Tottenham na Tottenham 0-1 Chelsea, bao la ushindi lilifungwa na Jorginho kwa mkwaju wa penalti.

Matokeo hayo yanaifanya Chelsea kufikisha jumla ya pointi 36 ikiwa nafasi ya sita baada ya kucheza jumla ya mechi 22 na Tottenham inabaki na pointi 33 ikiwa nafasi ya nane baada ya kucheza mechi 21.

Mourinho amesema: "Bado ninaona moyo wa upambanaji kwa wachezaji wangu wakiwa uwanjani, tupo pamoja na tunafanya kazi kwa pamoja hilo ni jambo jema kwangu na timu.

"Kingine ni hali ya kujiamini pia ipo, unajua ikiwa unashindwa kupata matokeo na timu yako inacheza vizuri kuna mambo ambayo ni lazima yafikiriwe ndani ya timu, ila sio mbaya kwa hapa ambapo tupo."

# Pires amtabiria Ramsey kurejea Arsenal

**LONDON, England**

ROBERT Pires anaamini kiungo wa Juventus, Aaron Ramsey 'atarudi' Arsenal siku moja na atakuwa makini kuendana na mfumo wa kocha, Mikel Arteta.

Ramsey amecheza michezo 20 ya ushindani msimu wa 2020/21, lakini ripoti nchini Italia zinadai Bianconeri hawaamini sana katika kumpa majukumu ya kwenye Uwanja wa Allianz.

Pires anaamini Ramsey tayari anafanya tofauti akiwa na Juventus na kwamba anaweza kuwa tegemezi wa Arteta.

"Anaendelea vizuri, kwa hivyo nimeridhika. Ushindani huku Juventus ni mbaya, kwa sababu kuna wachezaji wenye nguvu sana katika kila idara, " Pires alisema.

"Lakini kila wakati anacheza, anacheza kwa umakini sana, ana ufundi na mara nyingi anakuwa na nafasi nzuri ya kufunga, kama alivyofanya Jumamosi dhidi ya Sampdoria. Alifanya maamuzi bora.


"Ninaendelea kusema kuwa analeta mabadiliko hapa pia, kwa sababu sio rahisi kucheza kwenye safu ya kiungo na kuwa bora.


"Nadhani anaweza kuisaidia timu na kufanya maamuzi kama huko Arsenal.

"Namjua Andrea ni kocha chipukizi na nadhani anatafuta ni kwa namna gani kazi yake ni ngumu.

"Na ninatarajia anaweza kumtegemea Aaron, kwa sababu ni mchezaji mzuri na mtaalamu mzuri sana. Hilo ni jambo muhimu sana kwa kocha. "

Pires pia ameongeza kuwa timu yake ya zamani ya Arsenal inamkosa mchezaji kama Ramsey na akasema anaamini atarudi Uwanja wa Emirates siku moja.





# City yatamba itamsajili Haaland

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City inajiamini kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kwa pauni milioni 100, kwa mujibu wa ukurasa wa kwanza wa gazeti la Mirror la jana Ijumaa.

Haaland ni mmoja wa wachezaji ambaye anawaniwa na klabu mbalimbali barani Ulaya kwa sasa.

Amekuwa akuhusishwa kutakiwa na Real Madrid, Liverpool, Barcelona, Manchester United na Juventus.

**Lakini City ina imani yenyewe ndio yenye nafasi kubwa zaidi ya kumleta Haaland kwenye Ligi Kuu England.**

Haaland raia wa Norway amekuwa na wakati wa kuvutia sana pale Borussia Dortmund na anatajwa kwamba mmoja wa washambuliaji hatari zaidi wa baadaye.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAMTAKA RAMOS KUFUNGUKA

**Ni kuhusu hatima yake ndani ya klabu hiyo huku ikimpa muda hadi Machi, mwaka huu kufikia...**

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid inaonekana kuchoka kumsubiri, Sergio Ramos afanye uamuzi juu ya majaliwa yake ya baadaye klabuni hapo.

Na sasa Real Madrid imempa muda hadi Machi, mwaka huu kwa nyota huyo kutoa hatima yake na wao waendelee na hamsini zao, kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo.

Real Madrid wanataka suala hilo litatuliwe mara moja na kwa wote, kwani wapo kwenye maandalizi ya pambano la mtoano dhidi ya Atalanta katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mchezo ambao una umuhimu mkubwa kwa klabu hiyo.

Kwa sasa Ramos amewekewa mezani ofa ya nyongeza ya mkataba wa miaka miwili na punguzo la mshahara kwa asilimia 10 kutokana mlipuko wa janga la virusi vya corona kuathiri mapato.

Madrid hawatarajii kubadili msimamo huo, na minon'gono katika mji mkuu wa Hispania, Madrid ni kwamba wanaweza kumwacha Ramos aondoke huru mara mkataba wake ukimalizika ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Klabu hiyo imekuwa ikionyesha nia ya kumtaka nahodha wao abakie klabuni hapo, lakini ikiwa hatakubali ofa iliyopo mezani hakutakuwa na ofa nyingine.

Lengo la klabu ni kujua hatima ya nyota huyo mapema iwezekanavyo ili kujiwekea mipango kwa msimu ujao huku wachezaji kadhaa wakitarajiwa kutua hapo akiwamo, David Alaba.

Ramos ameonekana kuzivutia klabu za Manchester City ya Ligi Kuu England na PSG ya Ufaransa inayonolewa na Mauricio Pochettino.

## KWA UFUPI

**MESSI AIKANA CITY, PSG**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 33, hajafikia makubaliano ya mkataba mpya na klabu yoyote kati ya Paris St-Germain au Manchester City.

**SHVED AIKUMBUKA GENK**

WINGA wa Ukraine, Marian Shved mwenye umri wa miaka 23, amekubali alifanya makosa kujiunga na Celtic badala ya Genk. Shved sasa anacheza kwa mkopo kutoka Celtic. ***(Glasgow Live)***

**MBAPPE AITAKA MADRID**

KYLIAN Mbappe anataka kujiunga na Real Madrid, amesema Jese Rodriguez, aliyekuwa mchezaji mwenzake pale Paris St-Germain. ***(Marca)***

**NYOTA KUONDOKA INTER**

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Serbia, Aleksandar Kolarov mwenye umri wa miaka 35, na beki wa Italia, Matteo Darmian mwenye miaka 31, wote wanatarajiwa kuondoka Inter Milan msimu huu. ***(Gazzetta dello Sport)***

**TIMU EPL KUULA UEFA**

KLABU sita za Ligi Kuu England huenda zikacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kuanzia mwaka 2024. Mapendekezo ya Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), yatawezesha timu kucheza mechi 10 za makundi kila moja, huku kukiwa na uwezekano Ligi ya Europa ikapunguza idadi ya timu zitazoshiriki ligi hiyo.

**EN-NESYRI SOKONI**

KLABU ya West Ham inatarajiwa kutoa kitita kikubwa cha fedha kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Sevilla na raia wa Morocco, Youssef En-Nesyri ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Star)***

**MADRID KUMUUZA HAZARD**

KLABU ya Real Madrid inatakiwa kufikiria kumuuza kiungo wake raia wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 30, aliyekuwa mshambuliaji wa Bulgaria, Dimitar Berbatov ameweka wazi. ***(Betfair via Marca)***

**ROVERS YASAKA VIJANA**

KLABU ya Blackburn Rovers ipo katika majadiliano ya kufikia makubaliano ya muda mrefu na wachezaji wapya, akiwamo mshambuliaji, Adam Armstrong mwenye umri wa miaka 23, miaka michache ijayo. ***(Lancs Live)***

**WAN-BISSAKA MAJARIBUNI**

ALIYEKUWA mlinzi wa Manchester United, Fabio da Silva ameiambia klabu yake ya zamani kumsajili beki wa kulia mpya ili kumpa msukumo, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 23. ***(Manchester Evening News)***

**NICE YAPATA PIGO**

ALIYEKUWA kiungo wa Arsenal, Jeff Reine-Adelaide mwenye umri wa miaka 23, huenda akakosa mechi kwa kipindi kirefu baada ya kupata jeraha katika mishipa ya goti lake. Raia huyo wa Ufaransa anacheza Nice kwa mkopo akitokea Lyon. ***(RMC Sport)***

**ROBERTO MAJANGA**

KIUNGO wa Barcelona, Sergi Roberto mwenye miaka 28, huenda asishiriki mechi katika kipindi cha wiki sita bada ya kuumia na yuko katika hatihati ya kuikosa mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi Ulaya ya Paris St-Germain. ***(TV3 via Mundo Deportivo)***

HABARI MICHEZO

# MLANDEGE YAJIPANGA KUREJESHA USHINDANI

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege wamesema wamejipanga kuongeza nguvu katika kikosi hicho ili wafanye vizuri katika mechi za hatua ya lala salama ya ligi hiyo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mlandege, Ali Himid 'Kisoda' alisema matarajio yake ni kuona wanapata matokeo chanya katika mechi zinazofuata baada ya kufahamu kilichowaangusha katika mechi za mzunguko wa kwanza.

Kisoda alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana katika mechi zote zilizosalia ili kujinasua na janga la kushuka daraja.

Kocha huyo alisema moja ya maeneo ambayo watayafanyia kazi ni kusajili wachezaji wenye uwezo wa kukabiliana na mikimiki ya ligi hiyo ambayo msimu huu inashirikisha klabu 12.

"Tunajua hatua ya lala salama huwa ni ngumu na yenye ushindani zaidi, hata hivyo tumejipanga kuelekea hatua hiyo, tunataka kuziba mapengo kwa kusajili wachezaji watakaokuwa na uwezo wa kuhimili mshikemshike wa ligi, tunafahamu huko mbele ni pagumu zaidi," alisema Kisoda.

Aliyataja maeneo ambayo anatarajia kusajili wachezaji wapya ili kukiimarisha kikosi chake ni katika nafasi ya ulinzi na kiungo wa kati, ingawa hakutaka kuwataja nyota ambao wameanza mazungumzo ya kuwanasa.

"Tutaangalia wachezaji wazuri kutoka katika madaraja mbalimbali, tunataka kujinusuru na kushuka daraja, hivyo lazima tuzibe maeneo ambayo tunahisi yalikuwa na upungufu katika mzunguko wa kwanza, tunatarajia kusajili wachezaji ambao wataweza kucheza katika maeneo hayo," Kisoda alisema.

Aliongeza anaamini katika soka lolote linaweza kutokea, hivyo matokeo mabaya waliyopata katika mzunguko wa kwanza yakabakia historia na kurejea katika soka la ushindani.

"Hatukua na wakati mzuri, tumejipanga kumaliza tatizo lililopelekea mzunguko wa kwanza kufanya vibaya, ni kawaida ya mchezo kubadilika, pia siwezi kusema kama tatizo lilikuwa kwa wachezaji, kikubwa hatutaki kurudia makosa," Kisoda alisisitiza.



Mshambuliaji wa KMC FC, Charles Ilanfya (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Namungo, Steven Duah katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. KMC ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE**

# Kibo afikiria beji ya Fifa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWAMUZI Msaidizi, Ali Ramadhani 'Kibo', amesema ataendelea kufanya vizuri katika majukumu yake ili ndoto aliyonayo ya kupata beji ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) itimie.

Kibo ni mtoto wa aliyekuwa mwamuzi wa zamani wa Fifa, Ramadhani Ibada Kibo, ambaye kwa sasa ni kamisaa na mkufunzi wa ndani wa waamuzi visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kibo alisema anaamini ndoto yake itatimia endapo ataongeza juhudi na kuzingatia kwa usahihi mafunzo anayopata kutoka kwa wakufunzi wao.

Kibo alisema alianza kazi hiyo ya uamuzi akiwa na umri mdogo kwa kuchezesha mechi za vijana za madaraja ya chini, lakini sasa ni mwamuzi wa mechi za Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Kuu Zanzibar.

"Nimeanza fani hii nikiwa mdogo, niseme nimerithi kutoka kwa baba yangu japo yeye alikuwa mwamuzi wa kati na alipata beji ya Fifa, kazi hii naipenda kutoka moyoni ndio maana ninaonyesha juhudi zangu ili niweze kupata mafanikio," alisema Kibo.

Alitaja kikwazo anachokutana nacho ni kukosa nafasi ya kushiriki kozi mbalimbali zinazotolewa na Fifa kupitia katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa sababu Zanzibar hupeleka washiriki wachache katika mafunzo hayo.

"Katika waamuzi 19 wanaotakiwa kushiriki mafunzo ya Fifa hapa Tanzania, basi Zanzibar inaweza kupata nafasi sita au chini ya hizo, hii inakuwa hata ukishiriki unajiwekea matumaini ya kushindwa," Kibo alisema.

Aliongeza kwa kuamini bado siku yake haijafika na siku moja ndoto zake zitatimia.

## Ihefu FC yaandaa kampeni kujiokoa

**Na Saada Akida, DODOMA**

MABOSI wa Ihefu FC ya jijini Mbeya wamesema wamepanga mikakati imara ambayo wanaamini itawasaidia kubakia kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Ihefu FC, Juma Nyauba, alisema tayari wameshakubaliana kila mmoja kutimiza majukumu yake ili kufikia malengo yao ya kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mingine zaidi.

Nyauba alisema wameandaa kampeni maalumu ya kuhakikisha hawapotezi pointi katika kila mechi kwenye hatua hiyo ya lala salama ambayo itafanyika kuanzia Februari 13, mwaka huu.

Kiongozi huyo alisema kampeni ya kwanza waliyoiweka ni kuhakikisha wanashinda mechi zote za nyumbani na wanaamini hilo linawezekana endapo kila mchezaji atacheza kwa kiwango cha juu.

"Tayari uongozi kwa kushirikiana na Kocha Mkuu, Zuberi Katwila, tumeweka mpango kazi wa kuhakikisha tunabakiza pointi tatu nyumbani na kwenda kusaka alama moja ugenini, tuna imani tutajiweka katika nafasi nzuri kama kampeni hii itatimia vyema," alisema Nyauba.

Aliongeza maboresho waliyofanya katika dirisha dogo la usajili yameimarisha kikosi chao na sasa wanasubiri kuona malengo waliyonayo yanafikiwa kikamilifu.

Naye Katwila aliliambia gazeti hili bado ana imani na kikosi chake kitafanya vizuri katika mzunguko huo wa pili wa Ligi Kuu Bara kwa kucheza soka la kiwango cha juu katika kila mchezo.

Alisema mzunguko wa kwanza walikutana na vichapo vya mabao mengi kutoka kwa timu pinzani na safari hii wamedhamiria kutokuwa wanyonge na badala yake watalipiza visasi.

"Tumejipanga vizuri, hatushuki daraja, tutaingia katika mzunguko wa pili kupambana ili kutafuta pointi tatu, tutazuia pointi tatu kila mechi itakayochezwa kwenye uwanja wa nyumbani, na ugenini pia hatutalaza damu, huko ugenini tutakwenda na mkatati wa kutoa sare," alisema Katwila.

Ihefu yenye pointi 13 na inaburuza mkia, imeshinda michezo mitatu, imetoka sare mara nne na imekubali vichapo katika michezo 11.

# Michezo

Jumamosi Februari 6, 2021

Nipashe




## MADRID YAMTAKA RAMOS KUFUNGUKA

HABARI UK 22



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kulia), pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam, Barbara Gonzalez, wakitambulisha jezi mpya itakayotumiwa na Wekundu wa Msimbazi katika mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoanza baadaye mwezi huu. **PICHA: MTANDAO**

# GOMES AIPIGIA HESABU YANGA

●●●Mfaransa huyo anataka kuondoa tofauti ya pointi zilizopo dhidi ya watani hao ili...

**Na Saada Akida, DODOMA**

BAADA ya timu yake kupata ushindi katika 'kiporo' chake cha kwanza hapo juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema anahitaji kupata ushindi katika kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ili kupunguza idadi ya pointi walizotofautiana na watani zao na vinara wa ligi hiyo, Yanga.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa juzi dhidi ya Dodoma Jiji FC na kufikisha na pointi 38 baada ya kucheza mechi 16, huku vinara Yanga wenye pointi 44 wameshuka dimbani mara 18.

Gomes alisema mechi hiyo ilikuwa nzuri na yenye ushindani mkubwa, lakini wachezaji wake walicheza kiufundi na kimbinu zaidi katika dakika zote 90 na hivyo walifanikiwa kufikia malengo ya kuondoka na pointi tatu.

Mfaransa huyo alisema anaamini wapinzani wao walikuwa vizuri katika kipindi cha kwanza na kuufanya mchezo kuwa mgumu lakini alifanikiwa kubadili mfumo kwenye kipindi cha pili badala ya 4:4:2 na kuingia na 4:3:3 na hatimaye mipango yao ikafanikiwa.

"Ulikuwa mchezo mgumu, lakini tulijua kabla ya mechi kuwa mechi itakuwa ngumu, kipindi cha pili nilifanikiwa kubadili mfumo na kupata ushindi wa mabao 2-1, tumeridhishwa kwa sababu lengo kuu ilikuwa kupata pointi tatu na kupunguza idadi ya pointi sita kwa Yanga aliyeko kileleni," alisema Gomes.

Kocha huyo alisema sasa wanafunga ukurasa kuhusu Dodoma Jiji FC na wanarejea jijini Dar es Salaam kwa ajili kujianda kuwakabili Azam FC katika mchezo mwingine wa 'kiporo' wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Aliongeza kuwa hakushangazwa na kiwango kilichoonyeshwa na wapinzani wao kwa sababu alitarajia kukutana na ushindani huo kabla ya mechi haijaanza.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, wapinzani wetu walikuwa wanazuia vizuri, mabeki wao walikuwa hawaruhusu mianya ya mipira na walikuwa wakifika kwa wachezaji wangu kwa wakati, wanakaa nyuma, lakini wanafanya mashambulizi ya hatari kwa kutumia mawinga wao wa pembeni wenye mbio," Gomes alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Makata alisema timu yake ilicheza vyema katika kipindi cha kwanza na vijana wake walionyesha nidhamu nzuri iliyosaidia kuwazuia Simba kutofanya mashambulizi ya mara kwa mara, lakini dakika 45 za mwisho walifanya makosa yaliyowapa faida wapinzani wao.

**SIMBA KUTANGAZA UTALII**

Wekundu wa Msimbazi jana waliingia makubaliano rasmi na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya kutumia neno 'VISIT Tanzania' katika jezi zao mpya watakazozitumia kwenye mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wawakilishi hao wa Tanzania katika mashindano hayo wamefikia uamuzi huo kutokana na kutoruhusiwa kuvaa jezi yenye nembo ya SportPesa ambazo ni wadhamini washindani wa kampuni nyingine ya michezo ya kubashiri yenye mkataba wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

## YANGA, AFRICAN SPORTS KUKIWASHA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendelea kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wanatarajia kuwakaribisha Africans Sports katika mechi ya kirafiki itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz alisema jana kuwa mechi hiyo ni sehemu ya programu ya kiufundi iliyoandaliwa na Kocha Mkuu, Cedric Kaze katika kuwaongezea uwezo wachezaji wake.

"Tunayo sababu ya kukutana Azam Complex katika mchezo wetu wa kirafiki dhidi ya African Sports,... tunakwenda kuonyesha kikosi na ule upana ambao mwalimu Cedric Kaze alitaka kuonyesha ufundi kuelekea duru la mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, tufurahie kile kilichobora kutoka Yanga," alisema Nugaz.

Naye nahodha wa timu hiyo, Lamine Moro aliyekuwa majeruhi na kuikosa michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyofanyika Januari, mwaka huu amesema hali yake imeimarika na anatarajia kurejea dimbani katika mzunguko wa pili utakaoanza Februari 13, mwaka huu.

"Afya yangu imeimarika na napenda kuwaambia mashabiki watarajie kuniona kwenye ubora wa hali ya juu katika michezo ya duru la pili la Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Lamine.

Lamine aliliambia gazeti hili madaktari wake wamemruhusu kuanza mazoezi hivyo atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoendelea na kampeni ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo linashikiliwa na wapinzani wao.

Yanga ndio vinara wa ligi wakiwa na pointi 44 baada ya kucheza mechi 18, wakifuatiwa na mabingwa watetezi Simba yenye pointi 38, lakini imecheza mechi mbili pungufu ukilinganisha na watani zao.

Hata hivyo Yanga ambayo imeukosa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mitatu mfululizo, ndio timu pekee iliyomaliza mzunguko wa kwanza bila ya kupoteza mchezo, imeshinda mechi 13 na kutoka sare michezo mitano.

Mwadui FC ya mkoani Shinyanga, Mbeya City na Ihefu FC zote za jijini Mbeya ndio timu zinazoburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 18 za hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002